




**Wanafunzi** vyuo vya ufundi kukopeshwa fedha za HESLB

UKURASA 2





# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Mei 1, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580932

www.ippmedia.com

...com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




# CHADEMA waitwa maoni Katiba Mpya

• **Kikosi** Maalum cha Rais Samia chawaalika mezani, wenyewe watoa msimamo...*Endelea ukurasa 2*


## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

**BUNGE LAAGIZA KUANZISHWA KANZIDATA WAMILIKI MIGODI**

BUNGE limeiagiza Taasisi ya Uhamasishaji, Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi...

**UKURASA WA 5**

**MFANYABIASHARA TANZANITE KIZIMBANI TUHUMA ZA MAUAJI**

MFANYABIASHARA maarufu wa madini ya tanzanite jijini Arusha, Pendael Mollel (47), mkazi wa...

**UKURASA WA 8**

**TANZANIA, DRC ZASAKA FEDHA UJENZI SGR**

TANZANIA, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, zimewasilisha maombi ya kupatiwa mkopo weny...





Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan, akipiga kura kuwachagua viongozi wa Shina namba 1 la chama hicho, Chamwino Ikulu, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Mgogoro wa ardhi uliodumu miaka 23 watatuliwa

UKURASA 3

# LATRA yapandisha nauli za daladala na mabasi

UKURASA 2


**MICHEZO** **AZAM FC YALALAMIKIA UWANJA** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Kamati Kuu ya Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi, Mei Mosi Kitaifa 2022, wakati alipokagua maandalizi ya sherehe hizo, kwenye Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# CHADEMA waitwa maoni Katiba Mpya

**Na Romana Mallya**

KIKOSI Kazi cha Rais Samia Suluhu Hassan kimewaita wadau, kikiwamo Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kutoa maoni na mapendekezo katika maeneo tisa kinayoyashughulikia, likiwamo la Katiba Mpya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu wa Kikosi kazi hicho, Sisty Nyahoza, CHADEMA ambacho awali kilisusia kikao cha wadau wa siasa kilichofanyika Dodoma, ni miongoni mwa wadau kikiwa ni moja ya vyama vitatu vinavyotarajiwa kutoa maoni na mapendekezo yao Mei 9, mwaka huu.

**MSIMAMO CHADEMA**

Alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia suala hilo, Mkurugenzi wa Uenezi na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alisema:

"Kama ambavyo Kamati Kuu iliazimia kuhusu kutoshiriki mchakato huo, mpaka sasa hakuna uamuzi uliobadilika na tuna imani kuwa tutaweza kufanya mazungumzo kwanza ili tukubaliane tunaanzia wapi na ajenda za mazungumzo zitakuwa zipi.

"Tumemsikia Mheshimiwa Rais alipokuwa Marekani aliweka wazi kuwa ataendeleza mazungumzo hayo, nasi tutakuwa tayari kuendelea baada ya kuweka misingi ya mazungumzo husika."

Mbali na Katiba Mpya, maeneo mengine ambayo yanatakiwa kutolewa maoni na mapendekezo ni mikutano ya hadhara na mikutano ya ndani ya vyama vya siasa, masuala yanayohusu uchaguzi na elimu ya uraia.

Mengine ni mfumo wa maridhiano ili kudumisha haki, amani, utulivu na umoja wa kitaifa na ushiriki wa wanawake na makundi maalum katika siasa na demokrasia ya vyama vya siasa.

Rushwa na maadili katika siasa na uchaguzi, ruzuku ya serikali kwa vyama vya siasa na uhusiano wa siasa na mawasiliano kwa umma pia yanatakiwa kutolewa maoni na wadau hao.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, maoni na mapendekezo ya wananchi na taasisi katika maeneo hayo tisa yatapokewa jijini Dar es Salaam kuanzia Mei 5, mwaka huu hadi Mei 13, mwaka huu.

Ratiba hiyo pia inaonyesha Mei 5, mwaka huu watakaoanza kutoa maoni na mapendekezo ni Chama Cha Mapinduzi (CCM), kikifuatwa na Chama cha ACT-Wazalendo na baadaye Union for Multiparty Democracy (UMD).

Mei 6, mwaka huu itakuwa siku ya Chama cha Wananchi (CUF) na Chama cha NCCR-Mageuzi kutoa maoni yao na siku itakayofuata (Mei 7) ni Jumuiya ya Wahindu Tanzania na Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT).

Mei 9, mwaka huu, itakuwa nafasi kwa CHADEMA, Alliance for Demokratic of Change (ADC) na Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA).

Mei 10, mwaka huu, itakuwa nafasi kwa United Peoples Democratic Party (UPDP), African Democratic Alliance Party (ADATADEA) na Alliance for African Farmers Party (AAFP).

Taarifa hiyo inaonyesha Mei 11, mwaka huu watakaotoa maoni na mapendekezo ni United Democratic Party (UDP), Chama cha Demokrasia Makini (MAKINI) na Sauti ya Umma (SAU).

Siku itakayofuata ni National Reconstruction Alliance (NRA), Chama cha Kijamii (CCK) na National League for Democracy (NLD) na Mei 13, itakuwa ni nafasi ya Tanzania Labour Party (TLP) na Democratic Party (DP).

Taarifa hiyo pia ilibainisha kuwa maoni na mapendekezo yanapokewa kwa njia mbalimbali ambazo ni barua pepe, WhatsApp, barua na nyaraka yoyote kwenda kwa Katibu wa Kikosi Kazi.

Vilevile, inaruhusiwa wadau kuwasilisha barua au nyaraka husika katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa zilizoko Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar.

# LATRA yapandisha nauli za daladala na mabasi

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) imetangaza ongezeko la nauli za daladala na mabasi ya masafa marefu.

Viwango hivyo vipya vya nauli vilitangazwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Gilliard Ngewe na vitaanza kutumika rasmi baada ya siku 14.

Ngewe alisema kwa mabasi ya mjini kuanzia kilometa 0 hadi 10 nauli itakayotozwa itakuwa ni Sh. 500 badala ya Sh. 400 na zile zilizokuwa zikitozwa Sh. 450 zitakuwa ni Sh. 550.

Alisema kwa daladala zilizokuwa zinakwenda kilometa 20 nauli itakuwa Sh. 600 na kilometa 25 itakuwa Sh. 700, kilometa 30 nauli itakuwa Sh. 850 badala ya Sh. 750, kilometa 35 nauli ni Sh.1,000 na kilometa 40 nauli kikomo itakuwa Sh. 1,100.

Alisema katika safari hizo za daladala za mijini nauli za wanafunzi zimebaki zilezile.

Ngewe alisema kwa mabasi ya mkoani daraja la kawaida limeongezeka kwa asilimia 11.92 ambapo nauli itakuwa Sh. 41.29 kwa kilomita ambalo ni ongezeko la Sh. 4.40.

Alisema daraja la kati nauli ya sasa ni Sh. 53.22 kwa kilometa imeongezeka kwa asilimia 6.88 ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.66 kwa kila kilometa na kufanya nauli mpya iwe Sh. 56.88.

"Daraja la kawaida kwa mtu anayetoka Dar es Salaam kwenda Arusha kwa kupitia Chalinze nauli kikomo alikuwa akilipa Sh. 22,700, hivyo kwa sasa atalipa Sh. 26,700 na kwa daraja la kati alikuwa akilipa Sh. 32,800 na sasa atalipa Sh. 36,700," alisema.

Alisema kwa wanaopita Bagamoyo kwa ruti hiyo, daraja la kawaida nauli kikomo alikuwa akilipa Sh. 21,900 na kwa sasa atalipa Sh. 25,800 na kwa daraja la kati alikuwa akilipa Sh. 31,600 wakati sasa atalipa Sh. 35,600.

"Tumepandisha nauli kutokana na hesabu na ushindani kwa sababu kila mtu anajitahidi kutoa huduma, kubana mafuta, matumizi ya ovyo anajaribu kupunguza nauli haifikii kwenye kikomo.

"Kwa hiyo unatakiwa usiende ukaingia kwenye daraja la kawaida, ubaki kwenye daraja lako na wewe wa kati ubaki kwenye daraja lako, hatujasema uvuke, ukivuka ndiyo ugomvi unapoanza kwamba wewe unafanya kitu ambacho ni kinyume cha sheria," alionya.

Ngewe alisema kwa yeyote ambaye hataridhika na maelekezo hayo yaliyotolewa na bodi ya wakurugenzi na kudhani ipo haja ya kusikilizwa, anaweza kukata rufani au kuomba kuzikilizwa kwenye Baraza la Ushindani la Biashara.

# Wanafunzi vyuo ufundi kupewa mikopo HESLB

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema kwa mwaka wa fedha ujao wa 2023/24, serikali inatarajia kupanua wigo wa utoaji mikopo kwa elimu ya ufundi ngazi ya stashahada hususan kwa ujuzi na ufundi unaohitajika kwenye soko la ajira.

Akizungumza jana na Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), alisema katika kikao hicho wamezungumza umuhimu wa kupeleka mikopo katika elimu ya ufundi walau ngazi ya stashahada (diploma) kwenye vyuo vya ufundi hasa taaluma za ufundi na ujuzi ambazo zinahitajika sana kwenye ajira.

"Tunafahamu tuliongea na Balozi wa Canada alisema kampuni za madini za Canada zinataka sana tuweke aina fulani ya mafunzo ya kuandaa watanzania kupata ajira kwenye kampuni hizo, sasa watu kama hao tukiwapa mkopo uhakika wa kurudi ni mkubwa," alisema.

Prof. Mkenda alisema: "Kilio cha watu wengi kwa sasa ni ajira, sasa sehemu ambayo ajira ni rahisi zaidi ni kwenye ujuzi na ufundi, kwa hiyo vyuo kama DIT, Arusha Technical, tumekubaliana kazi ifanyike tuone mwaka mpya wa fedha, ukiacha mwaka huu tuwe tumejiandaa kupeleka fedha kwa ajili ya ufundi, tungependa tuseme mapema ili watakaotaka kuomba sehemu ya kusoma watambue sehemu hii sasa itakuwa na fursa ya kupata mikopo."

Kuhusu kutoa ufadhili kwa wanafunzi watakaofanya vizuri kwenye masomo ya sayansi, waziri huyo alisema katika bajeti inayotarajiwa kusomwa bungeni kwa mwaka wa fedha 2022/23, fedha zimetengwa kwa ajili ya wanafunzi hao kupata ufadhili moja kwa moja ambapo fedha hizo zitasaidia kusoma ndani au nje ya nchi.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkenda alisema itaundwa timu ya kupitia masuala ya utoaji mikopo kwa miaka mitano.

"Siyo kwamba tumeona tatizo bali kuna maswali mengi ambayo tunataka tusaidiane kuyajibu na bodi inataka kuyaona. Kwa mfano tunataka tujue wale waliochukua mikopo wanaorejesha, wanaorejesha zaidi ni waliosoma kozi zipi? itasaidia kujua iende sehemu gani zaidi, timu hii itaangalia pia vigezo kwa mfano, je, mtu amefaulu kwa kiasi gani? Maana kwa sasa inaangalia uwezo wa mzazi," alisema.

Kuhusu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG), Prof. Mkenda alisema CAG ameonesha namna ugawaji wa mikopo unavyokwenda na wamezungumza na bodi hiyo ambapo tatizo lilikuwa zamani lakini hadi sasa kuna uboreshaji mkubwa na juhudi zinaendelea.

## HABARI KITAIFA



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi (kulia) na Mkurugenzi wa Kampuni ya Tanzania Plantations Ltd, Ladhia Prabhudas Pradip, wakionyesha hati, baada ya kutiliana saini makubaliano ya makabidhiano ya mashamba ya kampuni hiyo na serikali, wilayani Arumeru, mkoani Arusha juzi. Waliokaa ni Waziri wa wizara hiyo, Dk. Angeline Mabula (wa pili kulia) na (wa tatu kulia), Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela. **PICHA: WANMM**

# Mgogoro wa ardhi miaka 23 watatuliwa

**Na Munir Shemweta,**
ARUSHA

SERIKALI imekabidhiwa mashamba yaliyokuwa yakimilikiwa na Kampuni ya Tanzania Plantations Ltd yenye ukubwa wa ekari 6,176.5 katika wilaya za Arusha na Arumeru mkoani Arusha na hivyo kumaliza mgogoro wa muda mrefu.

Mgogoro kati ya Kampuni ya Tanzania Plantations Ltd na Serikali uliibuka mwaka 1999 baada ya kampuni hiyo kupinga ubatilisho wa mashamba yake uliofanywa na serikali kutokana na kampuni hiyo kushindwa kutimiza masharti ya umiliki, jambo lililoifanya kufungua kesi Mahakama Kuu Kanda ya Arusha mwaka 2015.

Hata hivyo, katika kutafuta suluhu nje ya mahakama, serikali kupitia Wakili Mkuu wa Serikali, Mei 15, 2019 iliwasilisha ombi la kufanya majadiliano na mdai kwa lengo la kumaliza shauri nje ya mahakama ambapo mahakama iliridhia pande mbili za shauri kumaliza suala hilo nje ya mahakama.

Makabidhiano ya mashamba hayo yaliyokuwa yakijulikana kama Karangai na Lucy Estate yanahitimisha mgogoro kati ya serikali na Kampuni ya Tanzania Plantations Ltd sambamba na ule wa wananchi uliotokana na wananchi kuuziwa baadhi ya maeneo kwenye mashamba yaliyobatilishwa.

Katika makubaliano ya kutafuta suluhu nje ya mahakama, serikali ilikubali kulipa Sh. bilioni 5.7 kwa ajili ya fidia ya mashamba Na. 304 na 305 Nduruma yenye ukubwa wa ekari 6,133 na shamba la ekari 43.5 ambalo halikubatilishwa lakini ilionekana ni busara likachukuliwa na serikali. Pia serikali ililipa fidia ya mkonge na mtambo wa kuchakata mkonge uliokuwa ukifanya kazi.

Makabidhiano ya mashamba hayo yalifanyika juzi katika Kata ya Bwawani wilayani Arumeru mkoani Arusha baina ya Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi na Mkurugenzi wa Tanzania Plantation Ltd, Ladhia Prabhudas Pradip mbele ya Waziri wa Ardhi. Dk. Angeline Mabula.

Akizungumza wakati wa makabidhiano ya mashamba hayo, Waziri wa Ardhi, Dk. Angeline alisema Rais aliridhia makubaliano yafanyike na kutoa fedha kwa ajili ya fidia kumaliza mgogoro huo uliodumu kwa muda mrefu.

"Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa sababu masuala haya yanahitaji hekima na busara na aliliona hili kuwa kuna uhitaji wa kuwa na mazungumzo na Tanzania Plantation Ltd lakini pia akiangalia mustakabali wa watu waliokuwa eneo, tunamalizaje hili na kuelekeza makubaliano yafanyike na akatoa fedha na tayari mmiliki alishalipwa," alisema.

Kwa mujibu wa waziri huyo, serikali haiwezi kuwatelekeza wananchi waliokuwa wakiishi katika mashamba hayo na kubainisha kuwa itaweka utaratibu mzuri ili wananchi hao waweze kufaidika na matunda ambayo serikali imepanga.

Aliagiza halmashauri ambazo ni mamlaka za upangaji nchini kuendelea kufanya tathmini kwa yale mashamba ambayo wamiliki wake wameshindwa kuyaendeleza au kuyatelekeza na hatua za kuyatwaa zianze kufanyika mara moja. Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Dk. Kijazi, alisema Wizara yake kwa kushirikiana na wizara na taasisi nyingine imeanza kuchukua hatua zitakazoiwezesha serikali kufanya uamuzi kuhusu matumizi ya mashamba hayo ikiwamo uvunaji wa mkonge kwa kuzingatia baadhi ya mahitaji ya wananchi .

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, aliwatahadharisha wananchi wa eneo hilo kuwa eneo hilo sasa ni mali ya serikali na wanachotakiwa ni kusubiri utaratibu wa matumizi ya mashamba hayo utakapowekwa.

Kamishna wa Ardhi nchini, Nathaniel Nhonge, alisema kuwa baada ya makabidhiano ya shamba yaliyofanyika, ni lazima eneo hilo liandaliwe mpango wa matumizi ya ardhi kwa ajili ya manufaa ya nchi.

# EU, FAO na Serikali zazindua kampeni kuhimiza lishe bora

**Na Gerald Kitabu**

SHIRIKA la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Serikali ya Tanzania kupitia programu inayofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) inayoitwa AGRI-CONNECT zimezindua kampeni ya kitaifa ya lishe ili kujenga tabia zinazofaa za milo kwa kutumia vyakula vinavyopatikana nchini.

Kampeni hiyo iliyozinduliwa jijini Dar es Salaam jana inalenga kupunguza utapiamlo nchini.

Akizindua kampeni hiyo kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, Mkurugenzi wa Usalama wa Chakula katika wizara hiyo, Dk. Honest Kessy, alisema kipaumbele cha serikali ni kupunguza utapiamlo nchini.

Alisema kuwa kampeni hiyo imekuja katika kipindi mwafaka ambapo dunia inahangaika kumaliza janga la UVIKO-19.

"Tumeimarisha usimamizi wetu wa masuala ya chakula na lishe kwa kuhimiza uwekezaji zaidi katika kilimo, uzalishaji wa chakula na elimu ya lishe ili kuongeza upatikanaji na ufikiwaji wa milo iliyo bora kupitia uzalishaji katika kilimo na uelewa bora zaidi wa umuhimu wa milo bora katika kuzuia matatizo ya afya kwa sababu ya ukosefu wa lishe na kuimarisha kinga ya mwili," alisema.

Kessy aliwataka Watanzania wote kushiriki ipasavyo katika kampeni hiyo ili kupunguza tatizo la utapiamlo nchini.

Mwakilishi wa FAO nchini, Dk. Nyabenyi Tipo, alisistiza kwamba wakati janga hilo la dunia likiendelea, umuhimu wa milo bora katika kukabili madhara yake unapaswa kutiliwa mkazo.

Katika tukio hilo la jana, watu 100 wa kwanza kuwasili katika soko la Kisutu ulipofanyika uzinduzi huo, walipewa kikapu cha chakula kilichojaa vyakula anuai vilivyoonyeshwa katika sahani ya mfano ya milo bora. Mwezi huu wa Mei, kampeni kama hiyo ya lishe ya kitaifa itazinduliwa Zanzibar.

Programu hiyo inayoongozwa na FAO inayoitwa kujenga uhimilivu wa mifumo ya kilimo na chakula na lishe bora katika muktadha wa janga la dunia ni nguzo ya nne ya mradi wa AGRICONNECT-kusaidia minyororo ya thamani kuleta ustawi wa pamoja unaokazia zaidi lishe na kuanzisha mifumo ya kusaidia kupunguza makali ya janga katika upatikanaji wa chakula na masoko.


IN THE DISTRICT OF TEMEKE

AT ONE STOP CENTRE

PROBATE AND ADMNISTRATION
CAUSE NO. 309 OF 2022

In the matter of the state of the late AMINI NDAMA MZIRAY and in the matter of application for letters of administration by CAROLYNE AMINI MZIRAY

GENERAL CITATION
(rule 75)

All person claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate ( or letters of administration) is made to the above named petitioner

Objections to the grant should be filed on before the 6th day of 6th,2022

Dated at dar es salaam this 21 day of 4,2022

Registrar/Senior Resident Magistrate

XXXXXXX



KIWANDA CHA TAIFA CHA UCHAPAJI (KIUTA)

NPC KIUTA

MAADHIMISHO YA SIKUKUU YA WAFANYAKAZI DUNIANI - MEI MOSI 2022



Mhe. Dr. Hussein Ali Mwinyi
Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

Bodi, Menejimenti na wafanyakazi wa **Kiwanda cha Uchapaji cha Taifa (KIUTA)** tunaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Samia Suluhu Hassan** na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, **Mhe. Dr. Hussein Ali Mwinyi** na Watanzania wote katika kusherehekea Sikukuu ya Wafanyakazi Duniani.



Mhe. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Plot No. 13 Nyerere Road, Postal Address: Box 2320 Dar Es Salaam Tanzania
Tel: +255 22 2863216, +255 22 2863418, +255 22 2863209
Email: info@npckiuta.co.tz

216837702

# Nape aonya 'figisu' watumishi wizarani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye amewataka wafanyakazi wa Wizara hiyo kutokata tamaa wanapopitia magumu huku akiwaasa viongozi wao kutotumia ukubwa wa vyeo vyao kuwaumiza wengine.

Nnauye alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na wafanyakazi wa wizara hiyo.

Alisema watumishi hao wanapopata magumu katika majukumu yao hawapaswi kukata tamaa na kutaka watumie vikwazo kama fursa ya kupiga hatua mbele zaidi.

"Mfano mimi nilipokuwa ninafanya kazi katika ofisi za Makao Makuu ya CCM, nilisikia kuna mpango unasukwa na baadhi ya watu nihamishiwe mikoani, niliposikia nikaondoka kwenda kusoma 'masters' (shahada ya uzamili), nilipomaliza nilirudi na kuwashukuru wale walionihamisha, kila gumu ni fursa ya kufanya vizuri," alisema.

Aliongeza: "Ninaomba sana tupendane na tuishi kwa upendo, maisha niliyoyaishi yamenifundisha mengi kikubwa nawahimiza mtimize wajibu wenu".

Waziri huyo alisema viongozi wanapaswa kuwaeleza haki zao wafanyakazi taratibu na iwapo haiwezekani waambiwe kwa namna ambayo haitawapa msongo wa mawazo.

"Kila mmoja umpe haki yake, kama haiwezekani umwambie ukweli, tusidharauliane, tuheshimiane, tupendane na kuambiana ukweli," alisema.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Jim Yonaz, alisema ni muhimu kuwatengenezea wafanyakazi mazingira ambayo hayasababishi wapelekwe hospitalini.

Awali, akitoa mada ya magonjwa yasiyoambukiza, mtaalamu kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Jiji la Dodoma, Dk. Revocutus Baltazary, alisema asilimia 60 ya watumishi nchini wako katika hatari ya kupata magonjwa sugu yasiyoambukiza ikiwamo shinikizo la damu, figo na sukari.

"Sababu zinazotajwa ni mwenendo wa maisha wa kutofanya mazoezi, msongo wa mawazo na kutokuwa na usalama mahala pa kazi," alisema.

Aliwashauri watumishi kujenga utamaduni wa kufanya mazoezi, kula chakula bora na kuepukana na msongo wa mawazo.




Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, akizungumza wakati wa mkutano wake na wafanyakazi wa Wizara hiyo, jijini Dodoma jana. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Bunge laagiza kuanzishwa kanzidata wamiliki migodi

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

BUNGE limeiagiza Taasisi ya Uhamasishaji, Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI) kuharakisha kuanzisha kanzidata ya wamiliki wa migodi kwa maslahi mapana ya Taifa.

Pia limeiagiza serikali kuharakisha uandaaji wa mkakati wa kuendeleza madini ili kusaidia kutambua kiasi cha madini kilichopo nchini.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Seif Khamis Gulamali, alibainisha hayo juzi alipowasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2021/22 pamoja na maoni ya kamati hiyo kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Gulamali alisema ni wakati mwafaka sasa kwa TEITI kuanzisha kanzidata hiyo ya wamiliki wa migodi nchini kwa maslahi mapana ya Taifa.

Kuhusu mkakati wa kuendeleza madini, Gulamali alisema: "Ili nchi iweze kunufaika na rasilimali ya madini, wizara iharakishe uandaaji wa mkakati wa kuendeleza madini kama nchi nyingine zinavyofanya."

Alisema Kamati ya Nishati na Madini inatambua kuwa bado nchi haina mkakati huo na katika vikao vya uchambuzi wa bajeti kamati ilihoji suala hilo na kuarifiwa kuwa wizara iko kwenye mchakato wa kuandaa.

Gulamali ambaye ni Mbunge wa Manonga (CCM), alisema katika kuchambua, kamati ilipitia mikakati ya kuendeleza madini ya nchi na maeneo mbalimbali kama vile Ontario, Northwest na Yukon.

Alisema waliangalia namna zilivyojipanga katika kuhakikisha rasilimali ya madini inakuwa na manufaa kwa ustawi wa wananchi, lakini pia kunakuwa na mazingira mazuri ya uwekezaji.

Alisema kuwapo kwa mkakati wa kuendeleza madini kunalisaidia Taifa kutambua kiasi cha madini ambacho nchi imebarikiwa, lakini pia kuweka mipango na mikakati madhubuti pamoja na kuwajibika ili kuhakikisha rasilimali inakuwa endelevu na inatumika kwa ustawi wa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Gulamali alisema: "Kamati inaona ipo haja ya serikali kupitia mkakati wa kuendeleza madini wa nchi mbalimbali hususani zilizofanya vizuri ili kuweza kuiga yale mazuri kulingana na mazingira ya nchi yetu."

Kuhusu Mradi wa Makaa ya Mawe ya kupikia unaotekelezwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) eneo la Msasani, Dar es Salaam, Gulamali alisema ni moja kati ya miradi yenye faida kiuchumi na kimazingira kutokana na kuzalisha mkaa usiokuwa na moshi, harufu wala hewa chafu na wenye kuwaka kirahisi.

Alisema serikali inapaswa kuanza kutekeleza haraka, kikamilifu na kibiashara ili kuleta tija, pia kuna haja kwa serikali kushirikisha sekta binafsi ili kutekeleza miradi kama hiyo katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema utafiti pia utanyike ili mashine zinazotumika kutengeneza makaa ya mawe ya kupikia zianze kutengenezwa nchini kwa lengo la kupunguza gharama za uwekezaji wa mradi kwa kutumia wataalamu wa ndani.

**LESENI ZA BARUTI**

Awali Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko, alisema wizara imetoa leseni tatu kwa kampuni zitakazoanzisha viwanda vya kutengeneza baruti nchini.

Alizitaja kampuni hizo ni Mbogo Mining and General Supply Limited ya wilayani Magu mkoani Mwanza, Solar Nitrochemicals Limited na Emulsion ya wilayani Kisarawe mkoani Pwani.

Alisema leseni sita za kutengeneza baruti kwa kutumia magari maalumu zilitolewa kwa kampuni mbili pamoja na leseni 18 za maghala ya kuhifadhia baruti zimetolewa kwa kampuni na wafanyabiashara wa baruti.

Vibali na leseni za baruti vilivyotolewa zimeipatia Serikali Sh. milioni 453.05

Vilevile, alieleza kuwa katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 vibali vya baruti vilitolewa kwa kampuni na wafanyabiashara mbalimbali.

Alisema: "Serikali ilitoa vibali 225 vya kuingiza baruti nchini, vibali 21 vya kufanya biashara ya baruti, vibali 21 vya kusafirisha baruti kwenda nje ya nchi na vibali 37 vya kupitisha baruti nchini kwenda nchi nyingine".

# Wakunga waipa mbinu serikali vifo vya uzazi

**Na Sabato Kasika**

RAIS wa Chama cha Wakunga Tanzania (TAMA) ameishauri serikali kuwekeza zaidi katika kuboresha mazingira ya kazi na ubora wa vitendea kazi ili kupambana na vifo vinavyotokana na uzazi kwa lengo la kulinda afya ya mama na mtoto.

Feddy Mwanga alitoa rai hiyo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa warsha ya kuwajenga uwezo waandishi wa habari kuhusu masuala ya uzazi.

Alisema taarifa mbalimbali zinazotolewa na serikali na wadau mbalimbali zinaonyesha kuongezeka kwa hospitali na vituo vya afya, lakini kiwango cha vifo vya uzazi bado kiko juu nchini.

"Kuna haja kuongeza juhudi za kukabiliana na tatizo hili kwa kuhakikisha hospitali, vituo vya afya na zahanati zinakuwa na huduma zote muhimu ili kuepusha vifo vinavyotokana na uzazi," alisema Mwanga.

Alisema TAMA inatambua hatua kubwa ambazo Tanzania imepiga za kupunguza vifo vya mama na mtoto chini ya miaka mitano, lakini anashauri juhudi zaidi ili nchi ifikie lengo la maendeleo endelevu la asilimia 70 kwa vizazi 100,000 na kuondoa vifo vinavyoweza kuepukika kufikia mwaka 2030.

Warsha hiyo ilifanyika ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wakunga Duniani ambayo kilele chake kitakuwa ni Mei 5 jijini Dodoma na kutakuwa na kongamano la kisayansi, huku wakunga wakionyesha kazi wazifanyazo.

Naibu Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Afya, Uzazi na Idadi ya Watu (UNFPA) Tanzania, ambao waliandaa warsha hiyo, Dk. Wilfred Ochan, alisema Siku ya Wakunga Duniani ni nafasi ya kuangalia takwimu na jinsi uwekezaji ulivyo kwenye ukunga nchini. Alisema vifo vingi vinavyotokana na uzazi vinaweza kuzuilika, hasa kukiwa na huduma bora kutoka kwa wataalamu waliowezesha ili wasaidie kutoa huduma tangu mimba hadi mtoto anapozaliwa.

"Ripoti ya UNFPA kuhusu Shirikisho la Wakungwa na WHO inaonyesha kama serikali zikiwekeza kwa wakunga, maisha ya watu milioni 4.3 yanaweza kuokolewa kila mwaka kuanzia 2035," alisema Dk. Ochan. Alifafanua kuwa UNFPA inaendelea kufanya kazi pamoja na Wizara ya Afya na TAMA ili kuvuka malengo mbalimbali kuanzia uboreshaji wa vifaa tiba na wodi katika baadhi ya mikoa ikiwamo Kigoma.

Dk. Ochan alitaja mikoa mingine kuwa ni Dodoma, Simiyu na Zanzibar, huku akifafanua kuwa hatua walizochukua zinalenga kuwezesha kufanyika kwa huduma za dharura ikiwamo upasuaji.

# M'biashara tanzanite kizimbani tuhuma za mauaji

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MFANYABIASHARA maarufu wa madini ya tanzanite jijini Arusha, Pendael Mollel (47), mkazi wa Kiranyi na wenzake wawili, juzi walifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Arusha na kusomewa shitaka la mauaji ya kukusudia.

Washtakiwa wengine waliosomewa shtaka hilo ni pamoja na Onesmo Laizer (35), mkazi wa Ngaramtoni wilayani Arumeru ambaye ni mlinzi wa mfanyabiashara huyo na Deogratias Mollel (35), mkazi wa Sakina jijini Arusha ambaye ni mdogo wa mfanyabiashara huyo maarufu.

Akisoma shtaka la mauaji, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Grace Madikenya, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Arusha, Devotha Msofe, alidai kuwa mtuhumiwa Mollel na wenzake wawili walimuua kwa kukusudia Stephen Kivuyo (43) Aprili 18 mwaka huu katika eneo la Burka jijini Arusha majira ya saa 1.45 usiku.

Baada ya kusomewa shtaka hilo, Hakimu Msofe aliwaeleza watuhumiwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka kisheria kusikiliza kesi hiyo kwa kuwa ni ya mauaji.

"Kutokana na sababu hii washtakiwa hamtakiwi kujibu chochote hadi hapo mtakapopangiwa mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza kesi hii," alisema.

Hakimu huyo aliahirisha kesi hiyo hadi Mei 10, mwaka huu itakapokuja kutajwa tena.

# Madiwani walia na ubovu wa barabara

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga wamelalamika kuhusu ubovu wa miundombinu ya barabara wilayani humo unaosababisha kukwamisha shughuli za maendeleo.

Madiwani walitoa kilio hicho juzi kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani cha robo tatu ya mwaka wakati wakijadili taarifa ya Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA).

Walisema barabara nyingi wilayani humo ni mbovu na zinasababisha shughuli za maendeleo kutofanyika vizuri kutokana na kutopitika.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Ngassa Mboje, alisema ubovu huo wa barabara umekuwa ukichangia kuharibika kwa magari na kuwaingizia gharama za matengenezo pamoja na kutumia mafuta mengi.

Mwenyekiti huyo aliagiza TARURA kuwaondoa makandarasi wote ambao ni wazembe wanaotekeleza miradi ya barabara wilayani humo na kuweka wengine wenye uwezo.

"Makandarasi wote wababaishaji waondoeni, wanakwamisha miradi ya maendeleo, angalieni mikataba yao, fuateni taratibu na kuweka wengine ambao wana uwezo," aliagiza Mboje.

Kaimu Meneja wa TARURA wilayani Shinyanga, Salvatory Yambo, alisema kuwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22, kuna fedha zimeshatengwa kutengeneza barabara hizo na baadhi wameshapokea na kuanza utekelezaji.

Alifafanua kuwa fedha za ukarabati wa barabara ambazo zimetengwa kwa mwaka huo wa fedha ni Sh. bilioni 1.2 na wameshapokea Sh. milioni 973,9, fedha za barabara zitokanazo na maendeleo ya jimbo Sh. milioni 500 na wamepokea milioni 450; fedha zitokanazo na tozo ya mafuta ni Sh. bilioni moja na wamepokea Sh. milioni 637.



Ofisa Mnadhimu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, ACP Mkadam Mkadam, akitoa elimu ya usalama barabarani kwa waendesha bodaboda katika kituo cha mabasi cha Masasi, mkoani Mtwara juzi, alipokuwa safarini kuelekea jijini Dar es Salaam. **PICHA: A/INSP FRANK**

# Mhagama atoa maagizo saba mifumo TEHAMA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, ameagiza mambo saba kwa Wakuu wa Idara za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) serikalini ikiwamo kuimarisha mifumo ili kudhibiti upotevu wa mapato ya serikali.

Vilevile, amesema ni lazima taasisi zote za umma ziwasilishe na kupata kibali cha Mamlaka ya Serikali Mtandao kabla ya kutekeleza miradi ya TEHAMA ili kuondoa urudufu wa jitihada za Serikali Mtandao.

Mhagama alitoa maagizo hayo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kazi cha wakuu wa idara hizo.

Alisema bado eneo la TEHAMA linakabiliwa na vikwazo kadhaa vya kiutekelezaji ikiwamo kuwapo kwa mifumo isiyowasiliana au kubadilishana taarifa (ndani ya taasisi na kati ya taasisi na taasisi).

"Urudufu wa mifumo miongoni mwa taasisi za serikali yenye viwango na gharama tofauti zisizo na uhalisia, Huduma za Serikali Mtandao (e-services) kutowafikia wananchi wote hasa wa vijijini na kuongezeka kwa matishio ya usalama wa taarifa katika mifumo na miundombinu ya TEHAMA," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Mhagama aliagiza vikwazo hivyo vifanyiwe kazi haraka ikiwamo kuhakikisha sheria, kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao inazingatiwa na kufuatwa.

"Ninawaelekeza maofisa masuuli wote wa taasisi za umma kuhakikisha kuwa idara za TEHAMA katika taasisi zao zinaimarishwa na kuwa na watalaamu wenye weledi, vitendea kazi vya kutosha pamoja na muundo wa usimamizi wa TEHAMA unaokubalika," aliagiza.

Alisema Wakuu wa Idara za TEHAMA wa taasisi za umma ni lazima waweke na kutekeleza mikakati madhubuti ya namna ya kuzishughulikia kero hizo na kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao kwa pamoja.

Aliagiza matumizi ya mifumo shirikishi pale taratibu za utendaji kazi za taasisi za umma zinapokuwa zinafanana badala ya kila taasisi kuwa na mfumo unaojitegemea.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), Benedict Ndomba, alisema sheria ya Serikali Mtandao inahimiza kuwa na matumizi sahihi na salama ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na mifumo inayowasiliana na kubadilishana taarifa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua zichukuliwe dhidi waliotajwa ripoti ya CAG

**HIVI** karibuni, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali (CAG), Charles Kichere, aliwasilisha bungeni ripoti ya ukaguzi katika serikali kuu, serikali za mitaa na taasisi za serikali, ambayo ilibainisha madudu mbalimbali katika matumizi ya fedha za serikali.

Licha ya madudu hayo, Kichere alionyesha wasiwasi wake juu ya madeni yanayozikabili baadhi ya taasisi hatua ambayo aliweka bayana kwamba kuna uwezekano mkubwa zikashindwa kujiendesha na matokeo yake kuisababishia hasara kubwa serikali. Sambamba na madudu hayo, ripoti hiyo ya CAG imeweka wazi kwamba kuna utendaji mbovu na huduma zisizoridhisha katika baadhi ya taasisi nyeti ikiwamo Jeshi la magereza ambalo huduma za maji safi na salama ni mbovu.

Kutokana na ripoti hiyo, baadhi ya wadai wakiwamo viongozi, wanasiasa na wataalamu wabobezi katika masuala ya uwajibikaji, wameibuka na kutaka hatua zichukuliwe dhidi ya watu waliohusika upigaji wa mabilioni hayo. Inakadiriwa kwamba takriban Sh. trilioni 3.4 zimepotea kutokana na viashiria vya rushwa na ufisadi.

Taasisi ya WAJIBU chini ya mtendaji wake mkuu, Ludovick Utouh, ambaye ni CAG wa zamani, juzi katika mkutano wa kuchambua ripoti hiyo ulioandaliwa na Policy Forum. Iliweka bayana kwamba CAG ameonyesha namna matumizi mabaya ya fedha za umma yalivyokithiri katika ngazi mbalimbali za serikali na taasisi zake.

Sababu kubwa za madudu hayo, kutokana na WAJIBU, ni kutokuzingatiwa kwa taratibu za ununuzi na usimamizi wa mikataba, upotevu wa mapato kutokana na dosari za mifumo, miamala kufanyika mara mbili na kutofuatilia akaunti za benki. Naye Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema kuna haja serikali kuchukua hatua dhidi ya waliotajwa na CAG, vinginevyo kutakuwa na 'upigaji' mkubwa katika ripoti zinazofuata.

Alibainisha kuwa mwaka 2012 kulikuwa na ripoti kama hiyo ambayo ilitolewa na CAG, wakati huo akiwa Utouh, na kuibua mambo makubwa hatua ambayo ilisababisha mawaziri wanane katika serikali ya awamu ya nne chini ya Rais (mstaafu) Jakaya Kikwete, kuondolewa kwenye nafasi zao.

Ushauri huo wa Zitto umetolewa zikiwa ni siku chache zimepita baada ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, kusema waliotajwa kwenye ripoti hiyo hawana budi kuchukuliwa hatua.

Ni kweli wakati umefika kwa mamlaka za serikali, akiwamo Rais, kuitazama ripoti ya CAG iliyowasilishwa karibuni mbele yake pamoja na Bunge na kuchukua hatua stahiki. Kila mwaka ku kumekuwa na ripoti zinazoonyesha utendaji mbovu na usimamizi mbaya katika matumizi ya fedha za umma na matokeo yake miradi mingi kutokukamilika.

Wahenga wanasema ukicheka na nyani mwisho utavuna mabua, hivyo tunaamini kwamba kama mtindo huu wa kuacha kuchukua hatua kila ripoti za CAG zinapotolewa utaendelea, kuna uwezekano watu waliopewa dhamana katika nafasi mbalimbali wakajenga tabia sugu za kufanya maovu kama yalivyoainishwa. Matokeo yake serikali itaendelea kupata hasara huku wananchi wakiilalamikia kuwa haiwajali katika kuwaletea maendeleo.

Ni wakati mwafaka kwa Rais Samia Suluhu Hassan kuwachukulia hatua watendaji wote kama alivyosema Kinana na tuna matumaini kwamba atafanya hivyo kwa sababu kiongozi huyo aliweka hadharani kwamba atamshauri ili achukue hatua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Jamii ishiriki vita biashara haramu ya viungo vya albino

Na Sabato Kasika

**ZAIDI** ya miaka mitano iliyopita, soko haramu la viungo vya watu wenye ulemavu wa ngozi (albino), lilidhibitiwa na kuwafanya waishi kwa amani, lakini sasa dalili zinaonyesha kuwa huenda likarudi.

Hii ni kwa sababu ya kuanza kujitokeza kwa matukio ya mauaji kwa watu wenye ulemavu huo kwenye baadhi ya maeneo nchini, hali ambayo inaashiria kuwa inaashiria kurejea kwa soko hilo haramu.

Iko baadhi ya mifano ikiwamo ya mauaji ya mtoto wa miaka kati ya mitano hadi saba aliyedaiwa kuuawa mwaka jana mkoani Tabora, na mwili wake kuokotwa ukiwa umenyofolewa viungo ukiwamo mkono.

Tukio lingine linalohusisha imani za kishirikiana linadaiwa kutokea Novemba, mwaka jana, Lushoto mkoani Tanga baada ya watu wasiojulikana kufukua kaburi na kuchukua baadhi ya viungo vya marehemu.

Wakati matukio hayo yakiwa hayajasahaulika, limeibuka lingine Mabibo mkoani Dar es Salaam la mtu mwenye ulemavu huo kunusurika kukatwa mkono, hali ambayo ni wazi sasa kila mmoja wetu kuwa macho.

Takribani miaka mitano iliyopita, biashara hiyo ilikuwa ikisikika katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, lakini serikali ikafanikiwa kuidhibiti na sasa inaweza kuibuka upya hasa baada ya kuwapo baadhi ya matukio ya aina hiyo.

Ninaamini kwamba wananchi wakitoa taarifa kwa vyombo husika wanapoona dalili za kutaka kutokea matukio ya aina hiyo katika maeneo yao, huo ni ushiriki mkubwa wa vita dhidi ya biashara haramu ya viungo vya albino.

Pamoja na hayo, ni vyema wanaotaka utajiri kupitia viungo vya albino, wakatambua kuwa utajiri haupatikani kwa njia hiyo, bali ni kwa kufanya kazi kwa bidii, juhudi na maarifa.

Katika kukomesha biashara hiyo, ninaungana na kile ambacho kinapendekezwa na Kituo cha Sheria na Hakii za Binadamu (LHRC), ikiwamo kuiomba Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na asasi za kiraia kurudisha juhudi za pamoja za kukabiliana na vitendo hivyo kwa kuwa vinataka kujirudia.

Hatua hiyo inatokana na ukweli kwamba umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu, hivyo vita kukomesha biashara haramu ya viungo vya albino isiachiwe serikali na wadau wengine bali kila Mtanzania ashiriki.

LHRC ambao wameibua sakata la mkazi wa Mabibo Dar es Salaam mwenye ualbino kunusurika, wanapendekeza kuharakisha upelelezi wa kesi hiyo ili kukamata wahamasishaji wa soko hilo haramu la viungo vya albino.

Hapa wanaguswa waganga wa kienyeji na wanaoamini imani za kishirikina kwamba wachukuliwe hatua kali za kisheria ikiwamo kuwapa adhabu ambayo itakuwa fundisho kwao na kwa watu wengine.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, kukata viungo vya watu wenye ualbino ni kosa la jinai katika kifungu cha 225 cha Sheria na kanuni ya adhabu sura ya 16 kama ilivyofanyiwa mabadiliko mwaka 2019.

Ikumbukwe kuwa Juni 13 ya kila mwaka dunia huadhimisha siku ya kimataifa ya uelewa kuhusu watu wenye albino, maadhimisho ambayo ninadhani yangesaidia kuwabadilisha wanaofanya biashara ya viungo vya walemavu.

Umoja wa Mataifa kupitia baraza lake la tume ya haki za binadamu, lilipitisha azimio mwaka 2013 likitaka watu wenye ualbino walindwe na kuepuka vitendo vya unyanyapaa au mauaji dhidi yao.

Serikali imejitahidi kuhakikisha wanalindwa ikiwamo kuwatoa kwenye mazingira hatarishi na kuwaweka sehemu salama, ambapo kwa kipindi c ha zaidi ya miaka mitano, wameishi bila hofu ya kuuawa.

Wakati biashara hiyo haramu ikiwa imesahaulika vichwani mwa watu, zimeanza kuibuka dalili za kurejea upya, hali ambayo ni vyema kila Mtanzania kushiriki kikamilifu kuikomesha ili kundi hilo liendelee kuwa salama.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Wasiojulikana wameanza kutajana, Sasa jeshi la Polisi linangoja nini?



Na Pascal Mayalla

**Kwa muda mrefu, taifa letu limekuwa likisumbuliwa na kuhangaika na kundi la watu wanaoitwa "wasiojulikana", wanaofanya vitendo viovu ikiwa ni pamoja na utekaji, utesaji na mauaji na miili kutoonekana huku mingine ikiwekwa kwenye viroba na kutupwa mtoni, ziwani au baharini.**

NAOMBA kuanza hii makala yangu ya leo kwa msisitizo kwa kuuliza je, Jeshi letu la Polisi limefikia kiwango cha kushindwa kuwabaini watu wasiojulikana? Nimeanza na angalizo hilo, maana kule nyuma niliwahi kuuliza kama bunge letu linajipendekeza kwa serikali!

Niliitwa mpaka Dodoma na kuhojiwa na Kamati ya Kudumu ya Haki na Madaraka ya Bunge kwa madai eti nimetoa kauli ya kulikashifu na kulidhalilisha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusema linajipendekeza kwa serikali. Nilichowajibu ni kwamba sikutoa kauli bali niliuliza swali.

Mbunge aliyenituhumu bungeni, hakuiona alama ya kuuliza kwa kuwa sifa ya mbunge ni pamoja na kujua kusoma na kuandika, hivyo mtu yoyote aliyemaliza darasa la saba lazima ana uwezo wa kusoma na kuandika, hivyo uwezo huo wakusoma ni pamoja na uwezo wa kuiona alama ya kuuliza. Vitu vidogo vidogo kama hivi, vinatusababishia baadhi ya watu kuhoji viwango vya elimu vya baadhi ya waheshimiwa wetu huenda viko chini ya kiwango cha darasa la saba.

Kwa muda mrefu, taifa letu limekuwa likisumbuliwa na kuhangaika na kundi la watu wanaoitwa "wasiojulikana", wanaofanya vitendo viovu ikiwa ni pamoja na utekaji, utesaji na mauaji na miili kutoonekana huku mingine ikiwekwa kwenye viroba na kutupwa mtoni, ziwani au baharini. Baadhi ya miili iliyofungwa vibaya, huibuka juu ya maji na kuonekana ikiwa imefungwa kwenye viroba.

Miongoni vya watu waliofanyiwa uhalifu huo ni aliyekuwa Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Dk. Stephen Ulimboka; Mhariri Mtendaji wa zamani wa gazeti la Mtanzania, Absolom Kibanda;, mwandishi wa habari wa Mwananchi, Azory Gwanda; mwana Jamii Forums maarufu Ben Saanane, mfanyabiashara Mo Dewji na Roma Mkatoliki.

Vitendo hivi vilifika mahali pa kutisha zaidi na kwa kiwango cha juu pale aliyekuwa Mnadhimu Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Tundu Lissu, aliposhambuliwa kwa kumiminiwa risasi za kutosha, tena mchana kweupe akiwa katika makazi rasmi ya wabunge, yenye ulinzi imara saa 24 jijini Dodoma.

Kutokana na matukio hayo, hakuna mtu yeyote aliyewahi kushukiwa, kukamatwa au kuhojiwa wala jeshi letu makini na adilifu la polisi, halikuwahi kutoa taarifa yoyote ya uchunguzi wa matukio hayo. Hali hiyo ilisababisha kwenye mitandao ya kijamii, baadhi ya watu na taasisi fulani fulani kuanza kunyoosheana vidole kwa kuwataja baadhi ya watu na baadhi ya taasisi.

Taasisi ya kwanza kunyooshewa vidole ni Jeshi la Polisi lililoshutumiwa kwa madai ya kushindwa kufanya chochote kuzuia matukio hayo na baada ya matukio kutofanya uchunguzi wowote na kama walifanya uchunguzi kimya kimya, hawakutoa taarifa yoyote.

Ili tusizidi kunyoosheana vidole vya kushikana uchawi au kutafutana uchawi, kwanza nijitolea kuwafungua macho watu kuhusu hawa watu wanaitwa wasiojulika, wako wa aina mbili, wako "wasiojulikana" na 'wasiojulikana'. "Wasiojulikana" watakuja kujulikana, ila 'wasiojulikana', kamwe hawatakuja kujulikana ila kitu kinachoitwa karma kitawashughulikia kikamilifu.

Na kweli baada ya muda si mrefu, karma ilianza kula vichwa vya baadhi ya walionyooshewa vidole!, ila hawajaisha.

Kiongozi yoyote wa chama chochote au taasisi yoyote anapopata tip yoyote kuhusu uhalifu wowote, anapaswa kuripoti polisi. Kitendo cha kiongozi yoyote wa chama chochote kupokea taarifa yoyote ya uhalifu wa aina yoyote na kuinyamazia, kiongozi hiyo ni mashirika wa uhalifu.

Kama amepokea taarifa ya mipango ya uhalifu kabla haujatendeka na kuunyamazia bila kuuripoti, kiongozi ni mhalifu aitwae 'accessories before the fact'. Na kama kiongozi yoyote amepokea taarifa yoyote ya uhalifu wowote ulikwisha tendeka na akaunyamazia, huyu ni mhalifu aitwae 'accessories after the facts'.

Sasa baadhi ya wasiojulikana hawa wameanza kutajana!. Kiongozi mmoja mkubwa wa chama kikubwa cha siasa, juzi kati, aliibuka na kutoa siri ya wasiojulikana wa chama chake. Kiongozi huyu hadi ametaja tukio, aliyefanyiwa uhalifu na mhalifu aliyetenda uhalifu huo, badala ya kiongozi huyo kuripoti polisi, ameuzungumza uhalifu huo kwa vyombo vya habari.

Swali moja tu kwa jeshi letu makini na adilifu la polisi, linasubiri nini kumhoji asiyejulikana huyu ambaye sasa amejulikana awataje wenzake? Kama 'asiyejulikana' huyu, amewataja 'wasiojulikana' wenzake, je, Jeshi la Polisi linangoja nini kumhoji 'asiyejulikana' huyu?

**Paskali**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# TFF simamieni soka, tambueni pia viumbe



Na Joseph Kulangwa

**Aliumba bundi na hawa kunguru washenzi wa nini? Wanatusumbua na wengine kutugombanisha kishirikina tu hawana faida yoyote! Lakini ndio wameshaumbwa sasa, wana haki nao ya kuishi.**

TUNAELEZWA, tunakaririshwa na kuaminishwa kwamba vitu vya kwanza alivyoumba Mungu ni mbingu na ardhi au nchi, kisha tukafuata sisi na baadaye akaumba wanyama, ndege na wadudu.

Mungu akatwambia sisi watu kwamba twende duniani tukavitawale kila vilivyomo, akimaanisha tuamue kuvifuga na kuvila tukitaka, ilimradi tuendelee kuishi na kumwabudu.

Kilichosahaulika na ambacho sisi sote hatujui, ni kwamba yeye alitoka wapi, na kuja kutufinyanga sisi kwa udongo na kwa mfano wake yeye. Ina maana naye alitokana na udongo? Hilo ni fumbo.

Lakini itoshe tu kusema alipotuumba na kutukabidhi wanyama, ndege na wadudu, alifanya hivi kwa nia njema lakini akitaka nao viumbe hao waishi kama sisi. Yawezekana nao wana makanisa na misikiti yao wanakomwabudia kwa kuwaumba.

Ukifikiria sana utaona kuwa alikuwa na makusudi yake ya kutuumba sisi na viumbe hao wengine lakini tutajiuliza hivi aliumba nzi, viroboto, chawa, kunguni na nge, wa nini hawa? Kwa faida ipi?

Aliumba bundi na hawa kunguru washenzi wa nini? Wanatusumbua na wengine kutugombanisha kishirikina tu hawana faida yoyote! Lakini ndio wameshaumbwa sasa, wana haki nao ya kuishi.

Ukilinganisha mathalan nzi na nyuki, utaona utofauti wao ulivyo kifaida! Wote wanatua kwenye vitu vichafu na vilivyooza ndiyo, lakini mmoja ana faida, anatengeneza asali ambayo tunaila binadamu bila hata malipo, bali kikatili tu.

Kwa kifupi, kuna mahali tunatumia mabavu kuwaibia wadudu, wanyama na ndege kilicho chao kwa faida yetu, bila hata kugharimia. Huo ni wizi, ni uporaji na ni ukatili ambao unapaswa kukemewa.

Kwa muktadha huo huo, tunaona jinsi tunavyotesa wanyama, kwa kuwa tu ni wanyama. Kuna wakati nilipata kusema kuwa itakapotokea siku tukabadilishana na wanyama, itakuwa zamu yetu kunyanyasika.

Huo ndio wakati wanyama watakapohamia mijini nasi kuhamia maporini, wakaanza kutujangili kama tunavyofanya hivi sasa. Hatutakumbuka tulikokuwa, lakini cha moto tutakipata kama wanavyokipata wao hivi sasa.

Zamani nchini nakumbuka, kulikuwa na chama cha watu wanaotetea wanyama-TSPCA, sijui kiliishia wapi, lakini nadhani inda na choyo tulivyonavyo binadamu, ndivyo vilitufanya tukakiua kama si kukidhoofisha na kukosa kazi.

Hiki ni chama kilichokuwa kinahakikisha kuwa wanyama nao wana haki ya kuishi, wakila na kutunzwa kwa njia yoyote iliyo njema dhidi ya ukatili na magonjwa. Kilifanya vizuri sana.

Mtu au mfugaji aliyeonekana kutotunza mnyama wake, akimwacha azagae na kula ovyo au kuishi katika mazingira magumu, alichukuliwa hatua na kujirekebisha.

Tukielekezwa jinsi ya kumbeba mnyama au ndege, kuku asining'inizwe, wala nyau asikabwe shingo na hata mbuzi asifungwe kwenye kitako cha baiskeli na kusafirishwa, kwani nao wanaumia kama tunavyoumia.

Lakini leo tunajiuliza kulikoni? Nenda kwenye viwanja vya michezo husus̱an soka, utashitukia unamwona paka akikatiza, ujue huyo kaletwa na watu na kuachwa ama kwa makusudi au bahati mbaya.

Wengine wakitumika kishirikina au kutisha timu nyingine katika mchuano ili tu moja ishinde, lakini wengine wakifanya mbwembwe tu na wanyama au ndege hao.

Siku hizi utawaona mashabiki wamekuja viwanjani na kuku au njiwa, watawapeperusha na kuwapigia mikelele weee kuanzia mchana hadi usiku mechi zinapomalizika.

Kuku au njiwa huyo huko alikochukuliwa yawezekana hakuwa amepata kifungua kinywa na hawezi kuzungumza hivyo kwa kuwa yuko mikononi hawezi kufurukuta, atafanywa anayotaka afanyiwe bwana wake kwa muda wote huo.

Njiwa au kuku huyo muda wote kashikwa hana uhuru wa kukaa peke yake akatembea au kuruka au hata kunyoosha viungo, atabinywa huyo mpaka mbavu zitamwuma na atapumzika mechi imekwisha.

Na ikiwezekana anaweza kujikuta amekanyagwa, baada ya mmiliki wake timu yake kushindwa katika mechi na hivyo kupoteza maisha kwa furaha au huzuni ya mmiliki.

Hebu nasi binadamu tujifikirie, uchukuliwe nyumbani uwekwe kwenye kasha, muda wote unapigiwa kelele za mpira na hujanywa wala kula, itakuwaje? Kwa kuwa tu wanyama na ndege hawa hawana uwezo wa kutamka neno basi wanaonewa!

Hivi Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) haliwezi kufanya jambo kuzuia ukatili huu, unaofanywa na mashabiki dhidi ya wanyama na ndege hawa jamani? Lifanyike jambo hawa nao ni viumbe wa Mungu kama tulivyo sisi, haki sawa kwa viumbe wote jama!

**Alamsiki!**

## Ufaulu watoto kaya maskini waongezeka

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TATHMINI iliyofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa mwaka 2021, imeonyesha viwango vya ufaulu vimeongezeka kwa watoto wa shule za msingi na sekondari wanaotoka katika kaya maskini zinazofadhiliwa na mpango wa kunusuru kaya maskini chini kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Pia utapiamlo umepungua katika maeneo mbalimbali hapa nchini kwenye kaya hizo kutokana na wazazi kujitahidi kuwapa lishe bora watoto kupitia fedha za ruzuku wanazopata kupitia mfuko huo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya usalama na afya mahala pa kazi, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa TASAF, Zuhura Mdungi, alisema ufaulu huo umetokana na wazazi kuhamasika kuwapeleka watoto shuleni kupitia fedha za ruzuku tofauti na ilivyokuwa awali.

Mdungi alisema awali walipoanza kusaidia kaya hizo, hakukuwepo na mwamko wa wazazi kuwapeleka watoto shuleni kutokana na mazingira duni ambayo walikuwa nayo katika maeneo wanayoishi.

"Mradi huu umeonyesha mafanikio makubwa sana. Hata ukipita kwa walengwa unaona wamepiga hatua kutokana na hali walizokuwa nazo kabla ya kuingia katika mpango wa kunusuru kaya maskini," alisema. Mdungi pia alisema mwaka jana wamefanikiwa kupeleka wanafunzi 1,200 kutoka kaya maskini katika vyuo vya elimu ya juu ili kuendelea na masomo ambapo ni mafanikio makubwa kupitia ruzuku zinazotolewa na TASAF.

Akielezea wanavyohudumia wanufaika wa mpango wa TASAF, Mdungi alisema katika kipindi cha tatu tangu mwaka 2015 mpaka sasa, wana kaya za walengwa 1,275 na takribani watu milioni sita ambao wanahudumiwa kwa njia tatu.

Alizitaja njia ambazo hutumika kutoa huduma kwa walengwa hao ni pamoja kutoa ruzuku ya msingi ambayo hutolewa katika kaya zilizoko kwenye mpango pia katika kaya ambazo watu wanaweza kufanya kazi wanahudumiwa wakiwa ndani ya walengwa kwa kupata ajira za muda.

"Hawa wa ajira wanashiriki katika kazi za mazingira,ujenzi wa miundombinu ya maji, madarasa ambavyo huwasaidia kujipatia kipato na kukidhi mahitaji yao na familia," alisema Mdungi.

Alisema njia ya tatu ni kuwahudumia kwa kuhamasisha walengwa kuingia katika vikundi vya kuweka akiba ambapo hukutana na wenzao kwa ajili ya kubadilishana mawazo ikiwemo kujifunza ujasiriamali na baadae kuanzisha vikundi.

Kuhusu watoto wadogo, alisema wamekuwa wakiwahimiza wazazi na walezi kuwapeleka kliniki kwa ajili ya kupata chanjo pamoja na maelekezo ya namna ya kuwapa lishe bora ili kuepuka kupata utapiamlo. Mmoja wa walengwa wa mpango huo, Maleo Chisanza, kutoka kijiji cha Nagulo wilayani Bahi, aliishukuru TASAF kutokana na fedha ambazo wamekuwa wakipata kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya familia zao.

Alisema tangu ameanza kupata fedha za TASAF amepata mafanikio makubwa kutokana na kwamba hivi sasa anafanya ujasiriamali ambao unamsaidia kutunza familia yake ikiwemo kuwapeleka watoto shule.

# Tanzania, DRC zasaka fedha ujenzi SGR

**Na Benny Mwaipaja,** WASHINGTON DC

TANZANIA, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, zimewasilisha maombi ya kupatiwa mkopo wenye masharti nafuu Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Uvinza-Msongati hadi Gitega, yenye urefu wa kilomita 939, uliokisiwa kugharimu dola za Marekani milioni 900.

Majadiliano ya awali kati ya benki hiyo na Mawaziri wa Fedha wa nchi hizo, Dk. Mwigulu Nchemba wa Tanzania, Nicolas Kazadi wa DRC na Dk. Domitien Ndihokubwayo wa Burundi, yalifanyika juzi kando ya Mikutano ya Kipupwe ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mjini hapa.

Akizungumza baada ya kikao hicho, Dk. Nchemba alisema reli hiyo ni muhimu kwa ustawi na maendeleo ya kiuchumi ya nchi zote tatu kwa sababu itakapokamilika itarahisisha usafirishaji wa mizigo, abiria na kukuza biashara na maendeleo ya viwanda kwa nchi hizo.

Alisema mradi huo ni mkubwa ndiyo maana nchi hizo zimekubaliana kutafuta mikopo nafuu kutoka vyanzo mbalimbali na pia kwa kutumia fedha zitakazotengwa kwenye bajeti za ndani ili uanze kujengwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa AfDB Kanda ya Afrika Mashariki, Nnenna Nwabufo, alisema benki yake inatambua umuhimu wa mradi huo kiuchumi, kisiasa na kijamii na kwamba utasaidia pia kuziunganisha nchi zingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki na ni muhimu kwa ajili ya utengamano wa nchi hizo.

Aliahidi kuwa benki yake itashiriki kikamilifu kuhakikisha kuwa mradi huo unajengwa kwa manufaa ya wananchi wa nchi hizo pamoja na maendeleo ya kiuchumi ya nchi zinazoshiriki katika kujenga mradi huo muhimu.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (katikati), akijadiliana jambo na Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Nicolas Kazadi (kushoto), na Waziri wa Fedha na Uchumi wa Burundi, Dk. Domitien Ndihokubwayo, baada ya kikao chao na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Kanda ya Afrika Mashariki, Nnenna Nwabufo (hayupo pichani), kuhusu mkopo wa kujenga reli ya kisasa ya pamoja (SGR), katika Ofisi za Ubalozi wa Tanzania, Washington DC, nchini Marekani. **PICHA: WFM**

# Watendaji watakiwa kuzingatia maelekezo tathmini, ufuatiliaji

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, amewasisitiza watendaji katika taasisi za serikali kuzingatia maelekezo ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ya kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ili kuwa na mipango yenye tija kwa maendeleo ya taifa.

Akifunga kongamano la kwanza la ufuatiliaji na tathmini nchini lililofanyika katika ukumbi wa PSSSF, Makole jijini Dodoma, Ndejembi alisema Waziri Mkuu katika hotuba yake ya ufunguzi wa kongamano hilo alitoa maelekezo ya namna ya kuboresha masuala ya ufuatiliaji na tathmini pamoja na kongamano kwa miaka ijayo.

Alisema kwa kufanya hivyo watabaini nchi imepiga hatua kwa kiasi gani katika maendeleo na inakabiliana na changamoto zipi kufikia malengo na hatua za kuchukua kukabiliana na changamoto hizo.

Ndejembi alisema kongamano hilo lililenga kuwakutanisha watalaam na watendaji wa ufuatiliaji na tathmini wa ndani na nje ya nchi ili kujadili masuala ya ufuatiliaji na tathmini.

"Nina imani kuwa kupitia kongamano hili, mmepata fursa ya kubadilishana uzoefu na kuongeza uelewa kwenye masuala ya ufuatiliaji na tathmini. Uzoefu mlioupata uwe chachu katika kuboresha namna ya kusimamia utekelezaji wa majukumu ya ufuatiliaji na tathmini katika taasisi zetu," alisisitiza.

Ndejembi pia alizipongeza taasisi zote zilizopata tuzo na kutaka tuzo hizo ziwe chachu ya kuongeza uwajibikaji na kuzitaka taasisi zingine za serikali kufanya vizuri kwenye eneo la ufuatiliaji na tathmini si kwa ajili ya kupata tuzo tu bali kuimarisha utendaji kazi katika taasisi zao.

Kongamano hilo la kitaifa lililofanyika kwa mara ya kwanza nchini liliwashirikisha watalaam wa masuala ya ufuatiliaji na tathmini kutoka, mbali na Tanzania, Marekani, Uingereza, Ghana, Afrika ya kusini, Kenya, Uganda na Zimbabwe.

# MAISHA

MEI 1, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14

ONDOA SUGU

## Njia za asili zinaleta matokeo haraka



Ukurasa 15

MAISHA NI NYUMBA

## Namna ya kupangilia chumba cha kulala



Ukurasa 12

HARUSI





# Mapigo makali

Ukurasa 13

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | K | A | T | A | A |
| ■ | O | ■ | ■ | N | ■ |
| U | S | O | ■ | G | ■ |
| ■ | H | ■ | P | U | A |
| ■ | W | ■ | ■ | K | ■ |
| L | A | M | B | A | ■ |





## PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UMA, IGA, JANGA, JEMBE, BONGEA, JAMBIA

## CHEKA



Alichokifanya Adaktari

MTOTO Juma alikuwa shambani akimsaidia mama yake kupalilia mpunga. Wakati wanaendelea kulima ghafla alimuona chura akiruka ruka mbele yake. Juma alisimama akitafakari na kisha alikwenda na kunyanyua mguu akitaka kumpiga. Mama yake alimzuia na kumwambia kumuua kiumbe hai ni dhuluma na dhambi.

**Juma:** Mama mbona unanizuia kumpiga teke wakati na mimi nataka kumsaidia?

**Mama:** Hapana kumsaidia si kumpiga, ila msaidie kwa huruma

**Juma:** Mimi nilitaka nimtushe kulee, hata mwalimu alitufundisha kwamba Ukimpiga teke chura, humuongezea mwendo

**Mama:** Hapana huo ni msemo tu unamaanisha unapomuumiza mtu, humuongezea ujasiri na kuthubutu na sio kama ulivyoelewa wewe.

**SWALI**

Nyoka ana tabia ya kujiondoa gamba lake la juu, huchukua muda gani hadi hali hiyo huyokea?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mafanikio pasipo kumwamini Mungu ni kazi bure

***KARIBU tena msomaji wangu. Bado tunaangalia mambo yanayoua imani ya watu wengi. Wiki iliyopita nilijadili kipengele cha kuzoea hali ya kushindwa. Hiyo imetujengea tabia hasi kiasi kwamba hata ukipata uhakika toka kwa Mungu kwamba utashinda, unatilia mashaka.***

Leo nijikite kwenye kipengele kingine ambacho ni kule kutegemea nguvu na akili zako tu. Wapo watu wanaamini kwamba nguvu, akili, elimu, uzoefu wao vinatosha kuwapa mafanikio. Wote wenye tabia hiyo Mungu anawaonya kwa kuwaambia kupitia neno lake kwamba;

"Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha, nani awezaye kuujua?" Pia anasema kuwa "Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe".

Mwanadamu aliyeanguka dhambini anapoamua kujitegemea kwa mafanikio yake, maneno ya Mungu yanasema, moyo wake huwa ni mdanganyifu kiasi kwamba hajui kuwa anadanganywa na nafsi yake mwenyewe!

Msomaji wangu, inawezekana sana ukawafahamu watu wanaoonekana kufanikiwa pasipo kumwamini wala kumtegemea Mungu. Wakati wa Nabii Malaki wako watu walimlalamikia Mungu. Moja ya andiko likasema, "maneno yenu yamekuwa magumu juu yangu, asema Bwana. Lakini ninyi mnasema. Tumesema maneno juu yako kwa namna gani? Mnasema kumtumikia Mungu hakuna faida, na tumepata faida gani kuyashika maagizo yake. Na kwa kwenda kwa huzuni mbele za Bwana wa majeshi?

Na sasa twasema ya kwamba wenye kiburi ndiyo walio heri, naam, watendao uovu ndio wajengwao; naam wamjaribuo Mungu ndio waponywao? Kuna faida gani kufanikiwa pasipo kumtegemea na kumuamini Mungu?

Kujiamini nje ya Mungu ndiyo ishara sahihi kabisa ya mtu mwenye kiburi na haya ndiyo matokeo yake; Kiburi hutangulia uangamivu; Na roho yenye kutakabari hutangulia maanguko

Msomaji wangu, pamoja na kujiamini nje ya Mungu, wapo wanaowategemea wanadamu wenzao kwa mafanikio yao. Hawa nao wanaonywa, Mungu anasema, "Alaaniwe mtu yule amtegemeaye mwanadamu, amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake na moyo wake amemwacha Bwana."

Laana ni kinyume cha mafanikio. Na kumtegemea mwanadamu mpaka umfanye kuwa kinga yako hautafanikiwa katika maisha yako.

Eneo lingine linaloua imani ya mtu ni kule kuendekeza roho ya mashaka. Mungu anasema katika moja ya maandiko yake kwamba, "Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu awapaye wote kwa ukarimu wala hakemei;

"Naye atapewa, ila aombe kwa imani pasipo shaka yoyote; maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari lililochukuliwa na upepo na kupeperushwa huku na huku. Maana mtu kama yule asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana. Mtu wa nia mbili husita-sita katika njia zake zote."

Kuna aina ya watu hawamwamini Mungu, hawamwamini mtu yeyote na wala hawajiamini wenyewe. Kila kitu wanakitilia mashaka, ikiwa ni mchana hujificha wasionekane, ikiwa ni usiku wanasononeka kwa sababu hawaonekani. Ukiwasalimu wanajiuliza kulikoni na usipowasalimu ni shida!

Mashaka ni roho itokayo kuzimu hasa, na lengo lake ni kukunyima mafanikio ambayo Mungu amekwisha kukuandalia. Mashaka yakikuzoea huchukua mimba na kuzaa mtoto aitwaye 'woga'. Woga ndiye dereva wa gari liitwalo mashaka na safari hii hukupeleka kuogopa kivuli chako mwenyewe.

Eti huwezi kulala mpaka taa ziwe zinawaka, kisa unaogopa kukabwa, paka, bundi waliao usiku. Roho ya woga haikutoka kwa Mungu kama neno lake linavyosema; "Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi."

Hakuna mtu anayeweza kufanikiwa katika maisha kama bado anaburuzwa na roho ya mashaka na woga, kwani mapacha hawa hukufanya usimwamini Mungu. Maisha Ndivyo Yalivyo!

***Bila shaka msomaji wangu naamini umejifunza jambo hapo. Wiki ijayo nitajadi wivu na choyo, Usikose nakala yako ya Nipashe kila Jumapili. Je, una maoni au kisa cha kimaisha ungependa tujadili pamoja? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Machinga wanarejea, lazima kuwapo mipango thabiti

UNAPOTEMBELEA maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam, unaona namna wafanyabiashara wadogo wadogo wanavyoanza kurejea kwenye maeneo waliyoondolewa ambayo kimsingi hawatakiwi kufanya biashara huko.

Pia unaona baadhi ya waliopewa jukumu la kusimamia watu hao wasifanye biashara kwenye maeneo yasiyotakiwa kisheria, wakiwa sehemu ya kusababisha wawapo kutokana na kile kinachodaiwa ni kutoa 'kitu kidogo'.

Kwa sasa, ukitembelea maeneo kama Mwenge, Kariakoo na Buguruni, utaona kinachoendelea ambacho kinapingana na jitihada za kuwapanga watu hao ili kuhakikisha maeneo ya miji mikubwa nchini , ukiwamo Dar es Salaam, yanakuwa na mpangilio maalum.

Wako wanaotetea wafanyabiashara hao kuruhusiwa kufanya biashara kila mahali lakini kimipango miji ni lazima kupanga mji ili maisha yaendelee kwa kila anayeishi kwenye eneo husika.

Mathalani, kila barabara kuna watembea kwa miguu na vituo vya watumiaji wa usafiri wa umma. Kipindi cha nyuma maeneo hayo yalikuwa hayapitiki wala abiria hawezi kusimama kituoni kusubiri gari kwa kuwa liligeuka eneo la wafanyabiashara.

Lakini kwa Kariakoo paligeuka mahali pa serikali kupoteza mapato kwa kuwa machinga hawalipi kodi. Lakini kuna ambao walikuwa na bidhaa ambazo kimsingi ni sawa na duka linalopaswa kulipa kodi kiasi cha kupoteza ile dhana halisi ya machinga.

Kutokana na ongezeko lao walikuwa wanachukua bidhaa kwenye maduka na kuziuza mbele ya maduka hayo, kiasi cha wenye maduka ambao ndio walipakodi kukosa wateja. Wako waliokuwa wana mauzo ya zaidi ya Sh. 300,000 maana yake huyu ni sawa na mwenye duka.

Lakini wako waliofunga maduka na kubaki na maeneo ya kuhifadhia mizigo ambao kazi yao ni kuwauzia machinga ambao huuza kwenye mitaa mbalimbali.

Kwenye hifadhi za barabara, vibanda vilijengwa juu ya mitaro ya maji kiasi cha kukumbana na shida kutoka eneo moja hadi lingine, maana yake mpitanjia hana pa kutembea, hivyo analazimika kutumia barabara ya magari ambayo ni hatari kwa wengi.

Wakati machinga hao wanaondolewa, wengi walisema hii ni nguvu ya soda na kwenye maeneo mengi walisema watarejea baada ya serikali kusahau na ndicho kinachoonekana sasa wanaanza 'kujaribu' kurejea kama awali kwa kuweka bidhaa kidogo kidogo zinazobebeka kwa haraka.

Kila wilaya ilitakiwa kuja na mpango maalum wa kuwapanga kwenye maeneo maalum ambayo wengi hawayataki kwa kuwa wateja hawaendi huko. Kwingine waliwajengea kabisa vibanda ambavyo walianza kuvutumia na kukazoeleka.

Ongezeko la machinga linaonyesha hali halisi ya ugumu wa ajira za kueleweka. Kwa sasa vijana wengi wanamaliza vyuo vikuu na vya kati lakini hakuna ajira si serikalini wala sekta binafsi. Kama waliosoma hawapati ajira vipi kwa ambao hawajasoma kabisa?

Ukiwa kwenye foleni Dar es Salaam, utaona vijana wengi wanauza bidhaa za kila aina vikiwamo mapanga na visu huku wengine wakivizia gari linaposimama wanamwagia maji na kuosha kwa lazima. Unapokataa kutoa fedha wanalichafua au kama kioo kiko wazi wanakumwagia maji.

Hii yote inaonyesha bado kuna kazi kubwa katika kuzalisha ajira ili inapowekwa mikakati ya kupambana na machinga wanaongozeka kwa kasi mjini, wawe na kitu mbadala cha kuwaingizia kipato.

Lazima kujiuliza sababu zinazowafanya watoke vijijini au kwenye miji midogo kukimbilia mjini zinaweza kufanyiwa kazi ili wazalishe huko waliko na mjini kuwe mahali pa kuja kuchukua bidhaa tu?kwanini inashindikana?maana yake bado maeneo hayo hayajaendelezwa kukidhi mahitaji.

Wakati mwingine halmashauri zinazotakiwa kuwapanga watu hawa zinazidiwa nguvu. Mathalani kwa Dar es Salaam ambako maeneo mengi yamejaa wanapotakiwa kuwatengea maeneo inakuwa vigumu kwa kuwa huenda wanawapeleka pembezoni ambako wateja hawaendi.

Lakini huenda ubunifu unakosekana. Mara kadhaa ninapoandika suala la kuwapanga machinga huwa narejea mfano wa Jiji la Bangkok nchini Thailand ambalo limefanikiwa kuwa na majengo makubwa ambayo ndani yake kuna machinga wengi.

> **Kwa kuwa ni mjini basi wengi watakwenda kununua bidhaa kwa kadiri ya mahitaji yao kuliko kuwa na vibanda vya ovyo kila mahali ambavyo vinaharibu taswira ya mji.**

Unakuta limejengwa jengo kama la Mlimani City ndani yake kuna vibando vidogo vidogo vya mama lishe na machinga wa kila bidhaa. Maana yake mtu atakendwa huko kupata bidhaa za bei anayotaka. Ni mahali pa wafanyabiashara wadogo ambao ni rahisi kuwatambua na kuwaanzishia utaratibu wa kulipa mapato ambayo yatasaidia uendeshaji wa nchi.

Kama halmashauri zimezidiwa, eneo kama Karume linaweza kujengwa kwa muundo huo na kila mfanyabishara akapewa eneo lake. Kwa kuwa ni mjini basi wengi watakwenda kununua bidhaa kwa kadiri ya mahitaji yao kuliko kuwa na vibanda vya ovyo kila mahali ambavyo vinaharibu taswira ya mji.

Kama kuna waliofanikiwa na kupanga mji wao vizuri nasi tuige kwa kuwa wakiboresha halmashauri zitakuza vyanzo vya mapato na kupendezesha maeneo yao.

Bila kuwa na mipango inayotekelezeka na kuweka siasa kando suala la kupanga miji na majiji litaendelea kuwa kitendawili kwa kuwa watu wanaongezeka kila siku, uhamaji wa vijijini kwenda mjini kutafuta maisha ni mkubwa kuliko kutoka mjini kurudi kijijini.

## HARUSI







Magauni bora kwa bibi harusi ambayo yametengenezwa kwa kutumia kitambaa aina ya kitenge.





## MITINDO







# Mapigo makali

MACKENZIE ni aina ya nguo za zamani lakini mpaka leo zinapendwa kuvaliwa kutokana na umaridadi wake.

Vazi la Mackenzie linamng'arisha kila mtu na kumfanya awe na muonekano wa kupendeza.

Kwa wataalam wa masuala ya mavazi wanasema, nguo aina ya Mackenzie ambayo ina asili ya Wamarekani weusi inatokana na kujitukuza na kuthamini Uafrika zaidi.

Wanawake na Wanaume wengi wanapenda kuvaa vazi hilo ambalo limewavutia wabunifu, wameshona nguo maarufu duniani.

Kutokana na uzuri wa vazi hilo, baadhi wamefika mbali kwa kushauri Mackenzie liwe vazi la Taifa kutokana sifa yake kuu ya kuvaliwa na watu wa jinsia zote na kwamba halina tabu wakati wa kuvaa.

### VAA UPENDAVYO

Inapendeza sana kwa kushona gauni kwani inamfanya mwanamke kuonekana kama amevaa dera lenye maua mchanuo, kweli mvaaji anatoka bomba sana.

### SHATI NA SURUALI

Usijali Mackenzie inampa mvaaji mvuto wa aina yake pale anaposhona shati na suruali. Unachotakiwa kuhakikisha maua yanawekwa katika mpangilio mzuri.

### CHANGANYA NA KITAMBAA KINGINE

Baadhi ya watu wanashona gauni la Mackenzie kwa kuchanganya na vitambaa tofauti. Hilo halitoi maana ya vazi hili, bali linazidisha nakshi na kumfanya mtu kupendeza zaidi.

### VIKOI VYAKE BALAA

Kama vile haitoshi, unaweza kushona vikoi vya Mackenzie bila ya kuwa na wasiwasi. Mwana mama anayevaa gauni linalotokana na vikoi hana sababu ya kuchukia kwani inampa nafasi ya kutembea kwa madaha na furaha kwa sababu linamng'arisha sana.



ONDOA SUGU

# Njia za asili zinaleta matokeo haraka

MARA nyingi ngozi nyeusi kwenye kiwiko cha mkono ama goti husababishwa na mkusanyiko wa seli zilizokufa kutokana na msuguano sehemu hizo.

Kwa kawaida, sehemu hizi huwa kavu na hazina uwezo wa kutoa mafuta kama sehemu zingine za ngozi na hivyo zinahitaji kutunzwa na kufanywa kuwa safi.

Ukiwa na mazoea ya kuweka kiwiko chako kwenya meza wakati unapofanya kazi ama kukutanisha goti lako wakati unapofua, au shambani, ule msuguano hufanya ngozi yako katika maeneo hayo iwe nyeusi.

Hata hivyo kuna njia mbalimbali na rahisi za kuondoa weusi huo ambazo zimekuwa zikitumiwa na kina dada hasa nyumbani ambazo zinafanya kazi vizuri na kumaliza sugu.

**NDIMU**

Ndimu ina uwezo mkubwa wa kuzuia ngozi kuharibika na vitamini C ambavyo ni muhimu sana katika kuiboresha ngozi na kuifanya iwe laini tena.

Imethibitishwa kuwa ni kiungo muhimu katika kuifanya ngozi kuwa nyeupe.

Ina uwezo mkubwa wa kuzuia ngozi kuharibika na vitamini C ambavyo ni muhimu sana katika kuiboresha ngozi na kuifanya iwe laini tena.

Kwa kutumia pamba, kitambaa safi au tunda lenyewe tu, paka juisi ya ndimu iliyochanganyika na magadi kiasi katika sehemu zenye weusi.

Tulia nayo kwa muda wa saa moja kisha osha sehemu hiyo. Rudia kila siku hadi weusi utakapopotea.

**KIAZI**

Kiazi kina kimeng'enya ambacho kinasemekana kuwa na uwezo mkubwa wa kuondoa weusi kwenye ngozi bila ya kuongeza chochote.

Ukikikata na kupaka kwenye ngozi yako hasa maeneo ya kiwiko na goti kwa dakika 15 hivi, kabla ya kuosha kwa kutumia maji yenye joto kiasi, na kurudia siku kadhaa, kitaifanya ngozi yako kuwa nyororo na kusaidia kuondoa sehemu nyeusi.

**MAFUTA YA NAZI**

Mafuta ya kutokana na tunda hili yana vitu muhimu vyenye faida sana hasa vitamini E ambayo husaidia katika kurekebisha seli za ngozi zilizokufa au kuharibika.

Baada ya kuoga, unatakiwa kuupaka mwili wako mafuta hayo hasa maeneo unayohisi ni meusi sana na yanahitaji kufanywa kuwa meupe.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Hili ndilo biriani la Iddi

SIKUKUU ya Eid ndio hiyo imekaribia, unakosaje kupika biriani nyumbani kwako ukasherehekea vyema na familia yako.

Siyo kazi ngumu kuandaa na kupika biriani kama watu wengi wanavyodhani ni rahisi kabisa kama ambavyo nitatoa maelekezo.

**MAHITAJI**

Vipande vya kuku kilo moja, mchele wa basmati gramu 400, (unaweza kutumia mchele unaopenda), kitunguu maji kimoja, nyanya zilizokatwa tano, vitunguu saumu punje tano, pilipili za kijani nne na mafuta ya kula vijiko vya chakula vinne.

Mahitaji mengine ni mdalasini vijiti vinne, Hiliki vijiko vitatu hadi vinne, tangawizi iliyopondwa vijiko vya chakula viwili, majani ya nanaa yaliyokatwa, binzari nyembamba kijiko cha chai kimoja, chumvi kijiko cha chai kimoja, manjano kijiko cha chai nusu, zaafarani kijiko cha chai nusu (si lazima) na Kotmiri iliyokatwa robo kikombe.

**MATAYARISHO**

Loweka mchele wa basmati kwenye maji na uweke pembeni kwa dakika 15 hadi 30 (kama hutumii mchele wa basmati basi utaangalia mwenyewe mchele unaotumia.



**MAELEKEZO**

• Weka mafuta kwenye sufuria, yakipata moto kaanga kitunguu maji hadi viwe na rangi ya kahawia.

• Twanga kwa pamoja binzari nyembamba, kitunguu swaumu, tangawizi, nusu ya pilipili na vijiti viwili vya mdalasini, kisha weka kwenye vitunguu ukaange pamoja kwa dakika tatu.

• Tia nyanya na pika kwa dakika tano, tia vipande vya kuku koroga, acha iive kiasi cha dakika 10 hadi 15 na ikauke, weka pilipili zilizobaki kotmiri na masala ya kuku. Pika rosti liwe zito.

• Acha rosti na weka pembeni.

• Chemsha maji kwa hiliki na mdalasini na chumvi kisha weka mchele lakini usiive kabisa kwa dakika tano baada ya hapo mwagia maji.

• Panga wali na masala.

• Kwanza chemsha maji ½ kikombe katika sufuria utakayopikia biryani. Maji yakishachemka anza kuweka wali kisha rosti na malizia na wali. Kama una tumia zaafarani.

•Zaafarani kawaida hurowekwa kwenye vijiko vyenye maziwa ya vugu vugu na kumwagilia kwa juu.

• Weka moto mdogo kwa dakika 30. Baada ya hapo chakula chako kitakuwa tayari.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



## Jinsi ya kuchagua Wallpaper za ndani



WALLPAPER ni aina mpya ya upambaji ukuta katika nyuma, ambao husababisha kuwepo kwa mwonekano tofauti na unaovutia.

Je kama unataka kuweka Wallpaper una uzoefu wa kutosha kupata chaguo zuri? Basi kutokana na umuhimu wake tunakupatia baadhi ya dondoo ambazo zitakusaidia kupata chaguo zuri.

**1:** Wallpaper flati inakupa wigo mpana wa muonekano wa kung'aa na metaliki. Lakini kwa wengi hupendelea za michoro kuliko zile za flati.

**2:** Kabla ya kununua Wallpaper zingatia kiasi cha mwanga kwenye chumba husika kwa zile zenye rangi nzito au nyepesi ili kiwango kisiathiriwe.

**3:** Kama ni chumba cha kulala cha wanandoa, wallpapaer zenye maua ndiyo zinafaa zaidi kwani zinaleta hisia ya mahaba.

**4:** Kama ni sebule yenye mapambo ya mtindo wa kisasa, wallpaper zenye michoro ya rangi nzito, metaliki, ya kung'aa na ya mguso wa mtelezo ndio zinafaa.

**5:** Chumba kidogo kinapendeza wallpaper isiyo na michoro au maua, lakini kama unataka ya aina hiyo yawe madogo ili kuweka mandhari nzuri.

# Namna ya kupangilia chumba cha kulala

MPANGILIO mzuri wa chumba kwenye nyumba ni jambo muhimu sana na ni aina ya usafi ambao unachangia nyumba kuendelea kuwa bora na imara zaidi.

Kwa lugha rahisi ni kwamba unapopangilia chumba cha kulala kikawa katika mwonekano mzuri, unakuwa unaitunza nyumba yako. Baadhi yetu hufikiri kwamba chumba cha kulala kinaweza kupangwa pangwa tu pasipo sanaa na ubunifu wowote kwa sababu hakuna mgeni anayekwenda kuchungulia huko, la hasha!

Upangaji wa chumba cha kulala ni sanaa kama sanaa nyingine ya kawaida unayotumia katika kupanga sebule yako au kwenye mambo yako mengine muhimu na ukifanikiwa kutekeleza hilo kila siku hufurahisha nafsi yako mwenyewe na hata kwa ustawi kiafya.

Kwa wale wenye nyumba zenye nafasi, wana fursa kubwa zaidi ya kupangilia vyumba vyao kwa uzuri zaidi.

Miongoni mwa vitu muhimu kabisa unavyotakiwa kujua wakati unapangilia chumba chako, kwanza, unatakiwa ufahamu uelekeo wa kitanda chako kulingana na chumba chako kilivyo na baada ya hapo mambo mengine yatafuata.

Tunafahamu kwamba baada ya kuweka kitanda chako katika mwelekeo sahihi wa chumba uliouchagua, viko baadhi ya vitu ambavyo baadhi yetu huviweka humo, mfano kabati la nguo na vinginevyo.






Hili nalo linatakiwa kupangiliwa katika namna ambayo haliwezi kuharibu mvuto wa chumba.

Mwingine anaweza kupendelea kuweka zulia, hili nalo si baya kulingana na namna mtu anavyopenda mwenyewe, lakini pia linatakiwa kuzingatia rangi na 'size' yake.

Kwa wamama, wao wanapendelea chumbani kwao kuwe na 'dressing table'. Hii ni nzuri sana katika kupendezesha chumba hasa endapo itawekwa katika eneo sahihi. Lakini hii nayo endapo ikitumiwa vibaya hasa kuweka au kujaza vitu visivyo na umuhimu huharibu mvuto wa chumba.

Yako mengi yanayoweza kupangiliwa kwenye chumba na kuleta mvuto zaidi, lakini yote kwa yote, kinahitaji kufanyiwa usafi kila siku. Usafi huu ni pamoja na ule unaojumuisha utandikaji wa kitanda na shuka zilizo safi na kwa ustadi.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0713 447766
"MUTAEREWA TU!" WANAIZAYA NYIE!!!
JUKWAANI
SPESHO KUELEKEA IDD -EL- FITRI
...IVI KINACHOKUFANYA SIKUKUU ZOTE UKATAE KUTOKA WOTE KIPI?
"NGUMI ZAKO" NIKISALIMIWA NA KUPEWA OFA!
SIKUKUU NA MADEREVA WALIOKULA "MONDE"
SHERIA
HINYA!
AFWANDE HAYA MATOTO YAMESHASHIBA MAPIRAU "YANAMBIPU ZIRAILI" YAHESABIE KOSA MOJA KIRA YAKICHORA!... JUMURISHA NA MUSHIKAKI.
YAMESHA-CHORA MARA SITINI NA TISA NA BADO YANAENDEREA TWENDE NAYO SAMBAMBA.
WERAWERAAAA!!!
BICHI
..AFWANDE YAANDIKIE NA KOSA RA' KUTAKA KUJIWUA KWA MASUKUDI, HATA KAMA WASASI WAO WAJAWASITO!
KUDADAEKI!!! KUFUNGA WAFUNGE WENGINE, FURUGU WARETE WAO!!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
MAANDALIZI MEMA ...SIKUKUU NJEMA

HABARI KIMATAIFA

# Russia yazidi kushambulia usiku kucha

## ■Ukraine yadai imeshindwa kutwaa Donbass

**KYIV,** UKRAINE

VIKOSI vya Russia vimeshambulia jimbo la Donbass mashariki mwa Ukraine jana na kudaiwa kushindwa kufikia malengo yake.

Taarifa kutoka jeshi la Ukraine, ilisema Russia ilijaribu kuteka maeneo ya Lyman huko Donetsk na Sievierodonetsk na Popasna huko Luhansk.

Jeshi hilo lilitoa taarifa iyo wakati wa mkutano wake wa kila siku.

Kulingana na taarifa za ujasusi kutoka Ukraine, suala la kufanyika kwa kura ya maoni ili kuanzishwa kwa jamhuri katika mkoa wa Kherson kunaweza kupingwa na raia kutoka sehemu mbalimbali.

Russia ilisema jana vitengo vyake vya mizinga vimelenga maeneo 389 ya jeshi la Ukraine usiku wa Ijumaa na kuamkia jana ikiwa ni pamoja na vituo 35 vya ukaguzi, ghala 15 za silaha na risasi na maeneo kadhaa ambapo wanajeshi na vifaa vya Ukraine vimewekwa.

Wizara ya Ulinzi ya Russia ilisema makombora yake yaligonga maghala manne ya risasi na mafuta. Madai ambayo hayajathibitishwa na vyanzo huru.



Baadhi ya raia wa Ukraine wakilia baada ya kupoteza ndugu zao katika mashambulizi yanayoendelea yanayofanywa na Russia. **PICHA: BBC**

**UKRAINE YAISHUTUMU RUSSIA KWA KUIBA NAFAKA**

Naibu Waziri wa Kilimo wa Ukraine, ameishutumu Russia kwa kuiba tani laki kadhaa za nafaka kutoka katika eneo linalokaliwa na vikosi vyake.

Akizungumza kwenye televisheni ya Taifa ya Ukraine, Taras Vysotskyi, alisema anahofia kwamba Russia inaweza kuiba tani milioni 1.5 za nafaka katika maeneo ambayo sasa yanadhibitiwa.

Hata hiyo, Russia haijazungumzia madai hayo, lakini jeshi lake limekumbwa na hasara kubwa kiuchumi.

Mashambulio ya makombora ya Russia na hatua yake ya kuziba bandari ya Bahari Nyeusi ya upande wa Ukraine yametatiza uzalishaji wa nafaka, na kuzua wasiwasi wa kimataifa juu ya kupanda kwa bei ya vyakula.

Ukraine ni mojawapo ya wauzaji wa juu wa mafuta ya nafaka na mboga duniani. Imepewa jina la utani ghala la mkate la Ulaya.

Vysotskyi, aliwahakikishia wananchi wa Ukraine kwamba hawatakabiliwa na uhaba wa chakula kwa sababu ya usumbufu huo.

Meli ya mizigo iliyobeba zaidi ya tani 71,000 za mahindi ya Ukraine iliondoka kwenye bandari ya Romania ya Constanta siku ya Alhamisi na itakuwa ya kwanza tangu Russia ilipoivamia Ukraine Februari 24.

Constanta inashughulikia mauzo ya nje ya Ukraine kwa ishara ya Kiromania ya mshikamano, kwani jeshi la wanamaji la Russia linazuia eneo la Odesa,ambalo ni kitovu kikuu cha usafirishaji kwa nchi hiyo.

Nafaka ni suala nyeti sana nchini Ukraine, ambapo familia nyingi zina kumbukumbu za njaa ya miaka ya 1930, iliyosababishwa na uhamisho wa Sovieti wa wakulima matajiri na kuchukua mashamba.

**RUSSIA YAJIBU KAULI YA MAREKANI DHIDI YAKE**

Balozi wa Russia nchini Marekani Anatoly Antonov, amepinga shutuma za msemaji wa Pentagon John Kirby, kwamba Rais Vladimir Putin, alifanya ukatili katika uvamizi nchini Ukraine.

Juzi Kirby alionekana kuwa na hisia kali alipohoji jinsi mtu yeyote mwenye maadili angeweza kuhalalisha ukatili unaofanywa na Russia.

Lakini katika chapisho la mtandao wa kijamii, Antonov alielezea kauli ya Kirby kama ni ya kuudhi na isiyokubalika.

"Imekuwa kawaida maofisa wa utawala kuweka maamuzi yao juu ya uwongo mchafu wa mamlaka ya Ukraine," alisema Antonov.

Balozi huyo aliongeza kuwa kama Marekani haitaki uhasama ikomeshe chokochoko za Ukraine.

"Kilicho muhimu kwa John Kirby na wenzake ni kwamba kada ya kijeshi na viwanda vya Marekani vinapokea mapato ya ziada kwa kuondoa silaha za kizamani kutoka kwa maghala yao. Amepoteza heshima ya Ofisa wa Marekani, kwa kutumia matusi ya mitaani"aliongeza

**UJERUMANI YALAANI MASHAMBULIZI KYIV**

UJERUMANI imeikosoa Russia kufanya mashambulizi ya anga dhidi ya mji mkuu wa Ukraine, Kyiv wakati wa ziara ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres.

Msemaji wa serikali Wolfgang Buechner , alisema shambulio hilo si jambo la kibinadamu na wanalaani kwa nguvu zote.

"Tunalaani vikali shambulio la kombora la Russia dhidi ya Kyiv wakati Guterres alikuwa kwenye mazungumzo jana," alisema Buechner.

Russia ilithibitisha kuushambulia mji wa Kyiv jana usiku, lakini inadai kwamba lengo lake lilikuwa la kijeshi katika mtambo wa kutengeneza makombora.

Kituo cha utangazaji kinachofadhiliwa na Marekani cha Radio Liberty kilisema mmoja wa waandishi wake, Vera Hyrych, aliuawa katika shambulio hilo wakati kombora lilipopiga nyumba yake.

Vera Gyrych alikuwa nyumbani wakati kombora lilipopiga , kwa mujibu wa taarifa kutoka Radio Liberty.

Mwajiri wake alimuelezea kama mtu mwerevu na mkarimu, mahiri katika kazi yake.

Radio Liberty, pia inajulikana kama Radio Free Europe, ni shirika linalofadhiliwa na Marekani ambalo hutangaza habari katika maeneo mbalimbali duniani.

> **"Russia ilisema jana vitengo vyake vya mizinga vimelenga maeneo 389 ya jeshi la Ukraine usiku wa Ijumaa na kuamkia jana ikiwa ni pamoja na vituo 35 vya ukaguzi, ghala 15 za silaha na risasi na maeneo kadhaa ambapo wanajeshi na vifaa vya Ukraine vimewekwa.**

Hapo awali, meya wa Kyiv Vitali Klitschko, alisema mwili mmoja umepatikana baada ya shambulio la kombora la jana, ingawa hakuna maelezo zaidi ya mtu aliyeuawa yaliyotolewa wakati huo.

Wakati huo huo, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, ametoa ombi lingine la kutaka kuhutubia wakuu wa mataifa ya Muungano wa Afrika (AU).

Kulingana na Kamishna wa AU, Moussa Faki, alisema alipokea ombi wakati wa mazungumzo ya simu na Waziri wa mambo ya nje wa Ukraine.

Wawili hao walizungumza kuhusu Rais Zelensky kutaka kuendeleza uhusiano wa karibu na AU.

Faki hakufichua iwapo ombi hilo litakubaliwa, lakini alituma ujumbe wa twitter akisisitizia juu ya haja ya upatikaji wa suluhu ya amani katika mzozo wa Ukraine.

Mapema mwezi huu, kiongozi huyo alifanya mazungumzo kwa njia ya simu na Rais wa Senegal Macky Sall, ambaye ni Mwenyekiti wa sasa wa AU.

Nchi za Afrika zilitawala orodha ya mataifa ambayo yalijizuwia kupiga kura azimio la Umoja wa Mataifa la kuiondoa Russia katika baraza la haki za binadamu la Umoja wa Mataifa.

MAKALA

# HONGERA RAIS SAMIA, HONGERA TANZANIA



Na Magabilo Masambu - 0689157789

TANZANIA ni nchi yenye eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 947,303 ikijumuisha sehemu ya nchi kavu na majini kwa maana ya maziwa na mito. Katika nchi zilizomo katika jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Tanzania ni nchi kubwa kuliko zote. Hii ni kwa mujibu wa vitabu na machapisho mbalimbali yanayobainisha ukubwa wake katika ukanda huu.

Eneo kubwa la ardhi linatumika katika shughuli za kilimo na ufugaji, ambazo kimsingi ndizo shughuli hasa za kiuchumi, hivyo Tanzania inalo eneo kubwa la kutosha kwa wananchi wake. Upande wa maziwa na mito, mbali na maji kutumika katika shughuli za majumbani pia hutumika katika shughuli za uvuvi.

Maziwa kama Victoria, Nyasa na Manyara, hutumika kwa shughuli hizo. Tanzania huzungukwa na sehemu kubwa ya Bahari ya Hindi ambapo wananchi wake wanafanya shughuli za utalii pamoja na uvuvi.

Tanzania ni nchi yenye vivutio mbalimbali zikiwamo hifadhi za taifa ambazo ziko takribani 16 ambazo ni Arusha, Gombe, Katavi, Kilimanjaro, Mahale, Mikumi, Manyara, Ruaha, Rubondo, Serengeti, Saadani, Tarangire, Udzungwa, Kitulo, Mkomazi na Saanane. Mbuga hizi kila moja ina upekee wake. Mfano Manyara ni mahali pekee unakoweza kuwapata simba wanaopanda miti lakini pia ni mbuga pekee inayopatikana katika bonde la ufa. Katika mbuga hii, inapatikana pia chemchem ya maji moto.

Tarangile, hapa unakutana na tembo wengi zaidi kuliko mbuga zingine. Ni katika mbuga hii, unaweza kupata zaidi ya aina 500 za ndege kuliko mbuga zingine zote. Serengeti utakutana na wale wanyama watano wakubwa wanaitwa 'Big Five' yaani simba, tembo, chui, faru na nyati. Udzungwa, hapa ni mahali pekee unapoweza kupata aina 600 za miti isiyopatikana mahali popote duniani.

Gombe unawapata sokwe mtu ndiyo upekee wake na hifadhi ya Katavi inasifika sana kwa kuwa na mamba na viboko wengi zaidi kuliko mbuga zinginezo za taifa. Hifadhi ya Rubondo ni moja ya visiwa vilivyomo ndani ya Ziwa Victoria ambalo ni la kwanza Afrika na la pili duniani kwa ukubwa, kitu ambacho ni cha kipekee pia maana ni ziwa linalopatikana Tanzania. Ruaha ni hifadhi kubwa zaidi kuliko hifadhi zote Tanzania na hifadhi ya pili barani Afrika baada ya hifadhi ya Kafue iliyoko Zambia.

Tanzania ni nchi pekee katika bara la Afrika yenye mlima mrefu kuliko yote Afrika. Huu ni mlima mrefu kuliko yote duniani uliosimama kwa kujitegemea nao ni Mlima Kilimanjaro wenye urefu wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari. Mbali na mlima huu, iko milima mingine na mabonde ya kutosha pamoja na nyanda za juu kusini ambazo zinapendeza machoni mwa wageni na wenyeji.

Tanzania ni nchi ambayo mwaka 1992 ilibadili tambo zake za kisiasa na uongozi kutoka katika mfumo wa chama kimoja chenye nguvu zaidi na kuingia rasmi katika mfumo wa vyama. Msingi wa uongozi katika mfumo huu, wananchi ndio wenye mamlaka na viongozi wanapaswa kuwasikiliza wananchi. Imekuwa na utaratibu wa kubadilishana madaraka kwa amani toka awamu ya kwanza mpaka sasa.

Uhusiano wa kijamii ni jambo kubwa la kupigia mfano. Katika kujenga familia, Watanzania wanahusiana bila kujali makabila au dini zao. Mtu wa jamii yoyote, kutoka kabila lolote, anaweza kuoa au kuolewa na yeyote kutoka katika kabila lolote au dini yoyote bila shida. Hii ni tofauti na baadhi ya watu katika nchi zingine ambapo kabila au dini huwa ni kigezo kimojawapo kinachoweza kuzingatiwa wakati wa kuoa au kuolewa.

Amani na utulivu, nalo limekuwa eneo lingine ambalo Tanzania imekuwa nchi ya mfano katika jumuiya za kimataifa na Afrika kwa ujumla na kwamba imeongoza mapambano ya ukombozi hasa katika nchi nyingi za kusini mwa Afrika, lakini imesalia kuwa nchi yenye utulivu na amani toka kupata uhuru wake.

Ni moja ya nchi chache ambazo zilijipatia uhuru wake kwa njia ya amani bila mapigano na kufanya kuwa taifa la kipekee kama zilivyo nchi chache duniani maana nchi nyingi zimejipatia uhuru wake kwa njia za vita.

Mambo yote niliyoyasema hapo juu, lazima yapate mtu wa kuyasemea nje ya nchi hii na Rais Samia Suluhu Hassan amefanya kazi hiyo vizuri kabisa. Jambo moja muhimu ni kufahamu kwamba asingeweza kutangaza vivutio vya utalii pekee, lazima aseme kuhusu siasa na uongozi wetu na uhusiano wetu wenyewe ukoje.

Kwa hiyo si jambo la kubeza anastahili pongezi kubwa juu ya filamu aliyoicheza ya "Tanzania Royal Tour". Kwa namna yoyote ile, jambo hili litaleta manufaa kwa nchi tofauti na baadhi ya wakosoaji wanavyosema maana wageni wakija Tanzania hawaji kwenye familia ya Rais bali watakuja kutalii. Bahati nzuri serikali haimiliki kampuni za utalii kwani nyingi ni za watu binafsi, hivyo wanufaika wa kwanza ni hao.

Lakini wageni hao lazima waifahamu vyema nchi na kama tujuavyo biashara ni matangazo, hivyo hawawezi kuja kama hawajui kuna nini. Wako wanaohoji kwa nini uzinduzi wa filamu hiyo ufanyike Marekani? Hapo ni sawa kama amepiga jiwe katikati ya mzinga wa nyuki sasa tutegemee nyuki wasambae tujipange tu kukabiliana nao katika kutoa huduma nzuri.

Yale mambo ya baadhi ya askari barabarani ya kukamata magari yaliyopakia watalii na kuanza kuwasumbua, yaachwe kwani yanaharibu taswira ya nchi. Tumefundishwa kwamba mgeni akija nyumbani tunafunika tofauti zetu, akiondoka tunamalizana.

Niwapongeze Watanzania walioshiriki kuchangia utengenezaji wa filamu yenyewe lakini pia kwa namna tulivyoipokea katika uzinduzi wake uliofanyika Aprili 28 mjini Arusha. Tumuunge mkono Rais na kama kuna upungufu katika jambo lenyewe, tutoe ushauri kwa nia njema ili kusaidia likae vizuri zaidi kuliko kuishia kukosoa pekee.

**0689157789**
**ARUSHA-TANZANIA**
**magabilomjalifu@gmail.com**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Majina ya utani yalivyotamba kwenye soka



Na Adam Fungamwango

TUNAONA siku hizi wachezaji mbalimbali wa timu za Ligi Kuu wakipewa majina na watangazaji wa redio na televisheni. Mambo haya yalikuwapo tangu zamani. Tofauti ni kwamba kwa sasa ni wachezaji wachache tu wenye majina ya utani au wanayopewa kwenye soka tofauti na zamani ambapo asilimia kubwa walikuwa na majina hayo ya utani.

Labda inawezekana kwa sababu sasa wachezaji wenye uwezo mkubwa wa vipaji na kupambana uwanjani si wengi kama ilivyokuwa huko nyuma. Zamani wachezaji wengi walikuwa wapambanaji, hivyo wakapata majina kutokana na kufanana na kazi wanayoifanya uwanjani.

Hata wale waliokuwa na uwezo na vipaji, nao walipewa majina kutokana na jinsi walivyokuwa. Majina hayo walipewa na watu tofauti, kama si watangazaji mpira, basi ni mashabiki wa soka.

Ilipendeza sana kumsikia mtangazaji, alimtangaza mchezaji na kumtaja kwa jina lake alilopewa. Majina hayo yalikuwa yakiwakaa vyema kiasi kwamba huwezi kulitaja jina lake tu bila kutaja lile la utani.

Hata mtajaji mwenyewe ataona kama amelikosea, halijakamilika, au hakutendei haki. Moja kwa moja twende kwa majina hayo ya wachezaji na baadhi yao tutaangalia kwa nini walipewa majina hayo.

Idd Pazi, golikipa wa zamani wa Simba na Taifa Stars, alipewa jina la 'Father' na wachezaji wenzake kwa heshima kubwa waliokuwa nayo kwake, pamoja na uwezo wake. Hadi leo hii, hata mchezaji ambaye ni staa kwenye timu basi anaitwa kwa jina hilo.

Zamoyoni Mogella yeye aliitwa 'Golden Boy', alilopewa na kocha Mjerumani, Rudi Gutendorf aliyeifundisha Taifa Stars mwaka 1981, wakati huyo akiwa straika chupukizi wa Tumbaku ya Morogoro kabla ya kuhamia Simba mwaka huo huo. Alikuwa akifunga bao kila akiingia dakika 20 za mwisho kwenye michuamo ya Kombe la Challenge, kocha kaamua kumwita 'mwana wa dhahabu'.

Kulikuwa na beki mmoja wa kulia wa Simba anaitwa Daudi Salum, yeye alipachikwa jina la Bruce Lee kutokana na staili yake ya kuruka juu kwa ajili kupambana na mawinga hatari, akaitwa jina hilo la mfalme wa kungfu duniani.

Mohamed Kajole, beki wa kushoto wa Simba, yeye akapachikwa jina la Machela kutokana na aina yake ya uchezaji usio na mzaha. Ulisababisha mawinga wengi kuumia na kupandishwa kwenye machela kwenda kutibiwa mara kwa mara nje ya uwanja.

Beki wa kati wa Tukuyu Stars na Yanga, Salum Kabunda, alipewa jina la Ninja kutokana na aina yake ya kupenda kutumia nguvu zaidi kwenye ukabaji wake. Wakati mwingine akiruka miguu miwili. Aina hii ya uchezaji ndiyo anayo Abdallah Shaibu ambaye akapewa jina hilo hilo.

Said Swedi, straika wa Yanga yeye alipewa jina la 'Scud' kwani aliifunga Simba mara mbili kipindi ambacho kulikuwa na vita vya Ghuba mwaka 1990 hadi 1991 na ni makombora yaliyotumiwa sana na Iraq dhidi ya Marekani na washirika wake.

Kuna mchezaji wa Coastal Union, Razack Yusuph, yeye aliitwa 'Careca', ambalo ni jina mchezaji nyota wa Brazil wakati huo.

Said Mwamba akapachikwa jina la Kizota, ambalo ni jengo la mikutano la Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambalo lilitumika kwa ajili ya Mkutano Mkuu wa Tatu wa CCM mwaka 1987. Alipata umaarufu mwaka 1987 alipochezea timu ya mkoa wa Tabora katika michuano ya Kombe la Taifa na hatimaye kusajiliwa Yanga.

Wengine ni Celestine Mbunga 'Sikinde', Jobe Ayoub 'Kwasakwasa', Frank Kasanga 'Bwalya', Ally Malilo 'Loketo', George Lucas 'Gazza', Aboubakar Salum 'Sure Boy, Deo Njohole 'OCD', David Mwakalebela 'MP', Mohamed Yahya 'Tostao', Mohamed Bakari 'Tall', na Hamisi Gaga 'Gagarino.'

Wachezaji wengine ni Idd Selemani 'Meya', Haruna Moshi 'Boban', Michael Paul 'Nylon', Peter Lupokela 'Gari Kubwa', John Makelele 'Ziga Zig', Malota Soma 'Ball Juggler', Samli Ayoub 'Beki Mstaarabu', Mohamed Hussen 'Mmachinga', Itutu Kigi 'Road 'Master', Abbas Dilunga 'Sungura', Kitwana Manara 'Popat' na Makumbi Juma 'Homa ya Jiji'.

Pan African ilikuwa na beki mmoja wa kati akiitwa Rashid Idd, akipewa jina la Chama, lakini pia Yanga ilikuwa na beki wake wa kati akiitwa Athumani Juma ambaye naye akapachikwa jina la Chama. Walipewa jina hilo kutokana na uchezaji wao kufanana na aliyekuwa beki kisiki wa Zambia, Dick Chama. Huyu alikuwa beki wa kati katika timu ya taifa ya Zambia na Rashid na Athumani Juma walikuwa pia mabeki wa kati.

Hili jina lilikuwa maarufu sana nchini miaka ya 1980 hadi 1990, ambalo lilitokana na beki mmoja wa kati ya timu mbalimbali za Zambia na timu ya taifa, Dick Chama, miaka ya 1960 hadi 1970 aliyejipatia sifa kubwa kubwa kutokana na umahiri wake wa kupambana na mastraika wakorofi, ndiyo maana mabeki wengi vijana wakati huo wakajiita Chama.

Alikuwepo pia Boi Idd 'Wikens', Juma Pondamali 'Mensah' ambalo ni la kipa matata wa zamani wa Ghana, Robert Mensah.

Silvatus Ibrahim akaitwa Polisi, James Tungaraza 'Bolizozo' ambalo ni la mchezaji Jean Bolizozo wa Stella Abidjan aliyeifunga bao la pili kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Shirikisho mwaka 1993, ikilala mabao 2-0. Jina hilo akapewa mchezaji huyo wa Yanga.

Wengine ni Methord Mogella 'Fundi', Sanifu Lazaro 'Tingisha', Godwin Aswile 'Scania', Yusuph Macho 'Muso', Twaha Hamudu Noriega, Juma Mkambi 'Jenerali', Rajab Rashid 'Msingida', Bakari Malima 'Jembe Ulaya', Sunday Manara 'Computer', Salum Mwinyimkuu 'Carlos', Ally Yusuph 'Tigana' na Elias Michael 'Nyoka Mweusi'

Katika kundi hilo wamo pia George Kulagwa 'Best', Said Maulidi 'SMG', Mahmood Nyalusi 'Shilton', Ezekiel Grayson 'Jujuman', Mao Mkami 'Ball Dancer', Steven Mapunda 'Garincha', Omari Hussein Keegan', Maalim Salehe 'Romario', Abdul Ramadhani 'Mashine', na Ishaka Hassan 'Chukwu', ambalo ni jina la beki wa zamani wa timu ya taifa ya Nigeria Christian Chukwu.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

# Ajenda ya siri-28

**Na Adam Fungamwangwo**
**(0716 350534)**

AHSANTE, pole sana msichana mzuri, leo kwanza nenda nyumbani kapumzike, baada ya siku mbili nitakuja huko tuangalie jinsi gani tunaweza kufanya ili urudi shule ukasome, sawa?" Alimuuliza Tina akiwa anamshikashika kichwa chake ambacho sasa kilikuwa na upara.

"Kweli kaka?"

"Ndiyo, nitakulipia mimi ada, utaniambia unataka kusomea nini. Nikija Tandale kila kitu kitakuwa sawa, unasikia? Nadhani ukisoma baadaye unaweza kuondokana na mambo kama haya. Unaweza ukawa na akili ya kuanzisha biashara zako mwenyewe, kufanya kazi, au kujiajiri."

"Ahsate sana kaka 'angu, nimeambiwa na mama kuwa wewe ndiye umenisaidia hadi nimechiwa."

"Usijali mdogo wangu."

"Baba sijui mimi niseme nini, yaani mimi sina la kusema hapa, uuwiii..." Eddy alipoona Bi. Mtupeni ni kama mtu aliyepagawa, alimfuata na kumkumbatia. Halafu akamnong'oneza.

"Mama hapa watu wengi watakutazama, ngoja niite taksi kwa njia ya mtandao, iwarudishe nyumbani, halafu mimi niache hizi siku mbili, nitakuja huko tufanye tafrija fupi."

Akasalimiana pia na mumewe, akapongezwa kwa kazi kubwa. Kifupi ni kwamba eneo la Mahakama ya Rufaa lilionekana kama kuna sherehe fulani kutokana na kuachiwa kwa Tina.

Kila mtu alikuu akimkumbatia mwenzake ambaye anafahamiana naye, amekutana naye, au aliyekuja naye. Kila mmoja alionekana na furaha. Ni wachache mno ambao hawakuonekana na furaha. Walieleweka. Ni ndugu wa mke wa marehemu Chilambo, Hellen Kisa. Ndugu wa marehemu wenyewe walionekana kupigwa na butwaa, wasiamini kile kilichotokea. Awali walikuwa kundi moja, wote wakidhani Tina ni muuaji. Lakini baada ya hukumu, walitengana, ndugu wa mume na mke, kila watu walipita upande wao. Nje kulitaka kuzuka vurumai kwa ndugu wa pande wa mume kutaka kuwapiga wa mke, hasa akinamama, lakini watu waliamua. Wakatahadharishwa kuwa pale bado ni mahakamani.

Ndugu wa mume wakilaani vikali jinsi alichokifanya mke wa ndugu yao kuua, na kutengeneza mpango mkakati wa kuficha maovu yake. Ndugu wa mke wakiondoka haraka haraka kwa aibu, wakishindwa hata kuwatazama wenzao.




**Awali, Mahakama Kuu ilimhukumu msichana huyo kunyongwa hadi kufa kutokana na kupatikana na hatia ya kumuua Hafidh Chilambo kwa kumuwekea kwenye chakula aina mbili za dawa ambazo zikichanganywa zinageuka kuwa sumu.**

***************************

Alipowasha TV tu, kilichokuwa kikionekana ni kuanza kwa taarifa ya habari ya ITV, saa mbili usiku.

Na habari iliyokuwa kubwa siku hiyo ni hukumu ya mtuhumiwa wa mauaji Tina Kauzeni.

"Mahakama ya Rufaa imemuachia huru mtuhumiwa Tina Kauzeni mwenye umri wa miaka 18 aliyekuwa akituhumiwa na kesi ya mauaji ya bosi wake miezi sita iliyopita.

Awali, Mahakama Kuu ilimhukumu msichana huyo kunyongwa hadi kufa kutokana na kupatikana na hatia ya kumuua Hafidh Chilambo kwa kumuwekea kwenye chakula aina mbili za dawa ambazo zikichanganywa zinageuka kuwa sumu.

Hata hivyo, kesi hiyo ilikatiwa rufaa kwenye Makama ya Rufaa, na kusimamiwa na Wakili Florence Tinga hadi baadaye mtuhumiwa kuwa huru.

Taarifa zinasema kuwa mpelelezi maarufu nchini, Eddy Kamal, ndiye aliyefanya kazi hiyo ya kukusanya ushahidi na vielelezo visivyo na shaka ambavyo vimetumika kumuondoa hatiani mtuhumiwa.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi limewakamata mke wa marehemu Chilambo, Hellen Kisa na mtu mmoja anayefahamika kwa jina la Abdallah Mtola, kutokana na kushukiwa kuhusika na mauaji hayo.

Katika ushahidi uliomuondoa hatiani Tina, ambaye alikuwa ni dada wa kazi kwenye nyumba ya marehemu Chilambo, ni kwamba Hellen na Mtola wanaonekana kuhusika na mauaji hayo.

Jeshi la Polisi limesema kuwa litautumia ushahidi huo huo wa mpelelezi Eddy, kwenye kesi ya mauaji itakayofunguliwa hivi karibuni.

Imesema kuwa inafungua kesi kwa watu hao wawili ya kula njama kumuua Chilambo kwa kumuwekea sumu au dawa zilizogeuka kuwa sumu ili kumuua marehemu. Na sababu kubwa imeelezwa ni kwamba watuhumiwa hao wawili ni wapenzi, hivyo walikula njama hiyo ili kwanza Hellen arithi mali za marehemu mumewe, halafu kizuizi kiondoke, waoane. Walikuwa na ajenda ya siri.

Limesema kuwa watuhumiwa hao walifanya hila ili ionekane mfanyakazi wa ndani Tina kuwa muuaji, ili kuficha wao kujulikana."

Eddy alikuwa amekaa subuleni, akiwa amevaa pensi, kifua wazi akisikiliza na kuifuatilia kwa makini taarifa hiyo ya habari. Cha ajabu wakati ikitangazwa alionekana kama na yeye kushangaa kama mtu ambaye anayekisikia kisa hicho kwa mara ya kwanza.

Mwahija alitoka jikoni akiwa na kikombe cha chai, slesi mbili za mikate na mayai ya kukaanga. Akayaweka akampelekea Eddy.

"Mwanaume muongo wewe." Sauti ya Mwahija ilipenya vizuri kwenye masikio ya Eddy wakati akipiga funda la kwanza la chai.

"Kwa nini?" "Hivi uongo utakusaidia nini mwaya?" "Mbona sikuelewi Mwahija, nimekudangaya nini?"

"Kumbe Danny ndiyo Eddy Kamal?"

Sasa Eddy alijua kwa nini Mwahija aliongea hivyo.

Hakushtuka. Alijua Mwahija atajua kuwa yeye ni nani. Lakini hakutaka yeye kumwambia. Alitaka ajue mwenyewe.

"Danny ni jina la utoto, Eddy ni jina la ubatizo." "Na wewe kuwa mjomba wa Tina nayo imekuwaje?"

"Sina la kujibu, yote unayajua. Kama umeshajua mimi ni nani, basi nadhani umeshajua kwa nini sikukwambia mimi ni nani na kwa nini nilikwambia ni mjomba wa Tina."

Ni kweli Mwahija alijua kuwa mpenzi aliyenaye si Danny, bali ni mpelelezi maarufu nchini Eddy Kamal, wakati kesi ya Tina ilipomalizika. Aliwasikia na kuona watu wengi wakimzungumzia mahakamani hapo na kunyoosha vidole kwake, wakimshangaa na kumpongeza. Ni wakati akiwa ametoka na kuongea na Tinga, pamoja na watu wengine. Alishangaa, lakini alipoanza kurudisha picha nyuma tangu mwanzo alipomuona kwa mara ya kwanza kwenye famasi anayofanyia kazi, hadi kazi alizokuwa akitumwa kutafuta majina na walipo wafanyakazi wa nyumba ya marehemu Chilambo, picha ikaanza kumjia kuwa ni kweli, mpenzi wake hakuwa mtu wa kawaida. Na hata siku ya kwanza alipofika kwenye famasi anayofanyia kazi Tegeta, alikuwa yupo kazini kupeleleza na kusaka ushahidi wa kesi ile.

"Si ungeniambia mapema kama ni wewe ili nitambe kuwa nina mpenzi mpelelezi? Nilianza kukusikia na kukusoma zamani wakati nipo shule ya sekondari."

"Si umeshanijua, haya tamba sasa." Mwahija aliishia kucheka.

Ghafla, Eddy alimshika mkono wa kushoto Mwahija. "Fumba macho" Mwahija alishtuka. Lakini akafumba kidogo. Kuna kitu kilionekana kupenya kwenye kidole chake cha pili kutoka mwisho.

Akafumbua macho ghafla. Akapatwa na mshtuko mwingine. Safari hii ulikuwa wa furaha.

"Ha..., waooo." Alipiga kelele. Alimkumbatia kwa nguvu Eddy, nusura amwage na chai yenyewe. Kwa muda mrefu wakati amekaa pale alikuwa na pete mkononi. Alikuwa anataka Mwahija alete chai, ili amvalishe. Ilikuwa ni 'sapraizi' ya aina yake.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# NGOZI YA LULU DIVA MASHAKANI

MWANAMUZIKI Lulu Diva, amekiri kutumia sindano maalum ya kuongeza vitamin C ili kurudisha ngozi yake ya asili.

Lulu Diva amesema ngozi yake ilianza kuharibika baada ya kukithiri kwa matumizi ya dawa kali ya kutakatisha ngozi maarufu kama kujichubua ambayo ilimsababishia mikunjo na mabaka mwilini.

"Nilikuwa nang'aa sana wakati najichubua, lakini ilifikia wakati dawa ilianza kunikataa na kuaanza kutokea mistari na mabaka. Usichana uliniponza na pia nilikuwa sijikubali mwenyewe," amesema.

## BabaLevo unamchokoza Harmonize

MWANAMUZIKI na mchekeshaji, Baba Levo amembwatukia Harmonize akisema hana ubavu wa kumuingia Diamond katika mafanikio.

Baba Levo, amesema Harmonize bado sana kumfikia bosi wake wa zamani na kwamba hata kwenye kiganja cha Mondi hajai, licha ya kutembeza chuki dhidi yake.

"Harmonize hana uwezo wa kutengeneza kiki ya kumfunika Diamond Platnumz, kwa vyovyote vile hana uwezo wa kuzima EP ya FOA," amesema Baba Levo.



## Jennifer Kappic apanga kutikisa mitindo

MSANII na mwanamitindo anayekuja kwa kasi, Jennifer Inyasi maarufu kama Jennifer Kappic, ametamba kutikisa tasnia hiyo nchini kwa kutambulisha ubunifu mpya.

Mrembo huyo ambaye tayari amewavisha mastaa kibao wa Bongo Fleva, ameliambia Nipashe kuwa licha ya uchanga wake kwenye tasnia amekuwa akijizolea mashabiki wengi kila siku kutokana na kazi zake za kibunifu.

"Nimekuja kuichangamsha tasnia, naona hamna ushindani tena ndio maana hivi karibuni nitaleta ubunifu mpya ambao utazidi kunitambulisha. Nimefanya kazi na wasanii wengi na ninatamani niendelee kuwavalisha mastaa na watu wa kawaida ili kukuza jina langu," amesema.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LUKAKU ATAJWA BARCA

BARCELONA huenda wakaelekeza darubini yao kwa mshambuliaji wa Chelsea, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28, katika juhudi za kuimarisha safu yao ya ushambuliaji. Lukaku anaaminika kuwa mbadala wa Barca baada ya uhamisho wa Erling Haaland mwenye miaka 21 na Robert Lewandowski wa Poland mwenye miaka 33, kugonga mwamba. ***(Marca)***

### CITY KUMUUZA MAHREZ

KLABU ya Manchester City wanaweza kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Algeria, Riyad Mahrez mwenye umri wa miaka 31 msimu huu. ***(Give Me Sport)***

### ARSENAL, NEWCASTLE VITANI

ARSENAL na Newcastle United wamejiunga katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Juventus na Timu ya Taifa ya Argentina, Paulo Dybala. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 ataondoka Turin kama mchezaji huru msimu wa joto. ***(ESPN, via Mail)***

### PEPE AONDOKA ARSENAL

ARSENAL wamemtoa winga wao kutoka Ivory Coast, Nicolas Pepe mwenye umri wa miaka 2, kwa klabu nyingine ya Ligi Kuu England. ***(Express)***

### GUARDIOLA BADO AJIFIKIRIA

KOCHA Pep Guardiola hataharakisha kuongeza mkataba wake na Manchester City baada ya Jurgen Klopp kusaini mkataba mpya. Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 51 mkataba wake wa sasa unamalizika hapo mwakani. ***(Manchester Evening News)***

### FODEN MAMBO SAFI

KLABU ya Manchester City wanakusudia kurefusha mkataba wa kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Phil Foden mwenye umri wa miaka 21 hadi mwaka 2027. ***(Fabrizio Romano)***

### RANGNICK KUTUA AUSTRIA

MLINZI wa zamani wa Manchester United, Gary Neville amesema kocha wa klabu hiyo, Ralf Rangnick hapaswi kuchukua nafasi ya ushauri baada ya kukubali nafasi ya kuwa Kocha Mkuu wa Austria. ***(Sky Sports, via Express)***

### BELLINGHAM SOKONI EPL

LIVERPOOL huenda wakamnunua kiungo wa kati wa Borussia Dortmund mwenye umri wa miaka 19, Jude Bellingham, huku mikataba kadhaa ya wachezaji wao wa sasa ikielekea kumalizika. ***(Goal, via Express)***

### LOFTUS-CHEEK ASAKWA

KLABU ya Lazio inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Ruben Loftus-Cheek mwenye umri wa miaka 26. ***(Corriere dello Sport)***

### POTTER AMTAKA DUFFY

KOCHA wa Brighton, Graham Potter anakusudia kuzungumza na mlinzi wa Jamhuri ya Ireland, Shane Duffy kuhusu mustakabali wake msimu utakapokamilika. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2023. ***(Sussex Express)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP: LIVERPOOL NI TIMU SAHIHI KWANGU

**Kocha huyo asema hayo baada ya kusaini mkataba mpya wa kuendelea...**

**LIVERPOOL**, England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp anaamini kuwa ndio kwanza ameanza kutengeneza ufalme wake kwenye klabu hiyo baada ya kuongeza mkataba mpya.

Klopp amesaini mkataba mpya ambao utamweka kwenye klabu hiyo hadi mwaka 2026 huku akiwa kwenye kinyang'anyiro cha kuweza kushinda makombe manne msimu huu wakati katika Ligi Kuu England akiwa amebakiwa na michezo mitano, fainali ya FA, nusu fainali Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la Carabao ambalo tayari liko kabatini.

> **"Nadhani ni sehemu nzuri kuwapo au kujiunga, kama sio sehemu kamili-fu," alisema wakati akitoa uamuzi wa kuongeza mkataba mpya.**

"Dunia ipo kwenye kipindi kigumu, sio tu kwa corona, ni vita ya Ukraine, na mambo mengine mengi tu, na kisha muhimu kidogo mi usawa wa klabu kubwa kuwa na matatizo ya hapa na pale ya fedha.

"Tunataka kutoa hisia zetu, tunataka kutoa furaha, tunataka kuwa pamoja na watu wetu, tunataka tuungane kiukweli na tunataka kuwa watu wa tofauti pia kama klabu.

"Tutakaa kwa miaka 20 na tutaangalia nyuma na kutengeneza historia ambayo itakumbukwa kirahisi na kufikirika.

"Lakini inabidi tufanye sasa, hatuwezi kusubiri kwa miaka 10. Nimekuwa hapa kwa muda kidogo, na sio huu mkataba ambao tunakwenda kuangalia na kuondoka, hii ni nzuri, tukae hapa milele kwa sababu watu wanatupenda."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
WEST HAM
VERSUS
ARSENAL
1 | 4.08
X | 3.51
2 | 1.82

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RUDIGER RASMI KUJIUNGA MADRID



**MADRID,** Hispania

MLINZI wa Chelsea, Antonio Rudiger anatarajia kujiunga na klabu ya Real Madrid mwishoni mwa msimu huu kwa uhamisho huru.

Rudiger mwenye umri wa miaka 29, anatarajia kusaini mkataba wa miaka minne na Los Blancos hao, huku klabu za Manchester United, Barcelona na Paris Saint-Germain nazo zikiwa zinavutiwa na huduma yake.

Jumapili iliyopita, Kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel alithibitisha kuondoka kwa mchezaji huyo kwenye dimba la Stomford Bridge kutokana na kuwekewa vikwazo dhidi ya mmiliki wa klabu hiyo, Roman Abramovich ni moja ya sababu kuu ambayo ilipelekea kushindwa kumwongezea mkataba wake.

Rudiger ameitumikia Chelsea kwa muda wa miaka mitano baada ya kusajiliwa kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 29 akitokea nchini Italia kwenye klabu ya Roma.

Muda alioutumia akiwa na Chelsea amefanikiwa kushinda Kombe la FA, Ligi ya Europa, Ligi ya Mabingwa Ulaya (2021) ,taji la Klabu Bingwa Duniani na Kombe la UEFA Super.

Msimu huu Rudiger ameichezea Chelsea michezo 47 katika mashindano yote, huku kwenye timu yake ya taifa ya Ujerumani amechezea michezo 50.



## *Conte afunguka kuhamia PSG*

**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte amepinga vikali kuhusu taarifa ambazo zilikuwa zinazagaa za kumhusisha kutaka kuhamia kwenye timu inayoshiriki Ligi Kuu Ufaransa, Paris Saint-Germain na kuita uvumi huo ni habari za uongo.

Conte amejiunga na Spurs Novemba mwaka jana lakini tayari amehusishwa na kutaka kutimka kwenye klabu hiyo yenye makazi yake London Kaskazini, huku taarifa kutoka vyombo vya habari vya Ufaransa zikidai kocha huyo anataka kazi ya kuinoa PSG.

Kwenye kikao chake na waandishi wa habari kabla ya mchezo wake wa leo Jumapili dhidi ya Leicester city alinukuliwa akisema, “bila shaka, nadhani ni jambo zuri kwa klabu nyingine kuipenda kazi yangu, hili ni jambo moja.

“Lakini ukweli ni kwamba sipendi watu wanapojaribu kubuni habari, kwa kuzungumza tu, kutengeneza tatizo. Hii sio sawa, na sio haki kwangu, kwa klabu na kwa wachezaji wangu.

‘Pia kwa sababu akili zetu kwa sasa zipo kwenye hii michezo mitano kupata matokeo mazuri kwetu.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# SERENGETI GIRLS DIMBANI, YANGA PRINCESS YANYWEA

Na Saada Akida

WAKATI kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), kinashuka dimbani leo kuwavaa Burundi, nahodha wa Yanga Princess, Amina Bilali amesema klabu yake imeshajiondoa katika vita ya ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

**Serengeti Girls inaikaribisha Burundi katika mechi ya marudiano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia (U-17), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar.**

Katika mechi ya kwanza iliyofanyika kwenye mji wa Ngozi,Burundi, wawakilishi hao wa Tanzania walipata ushindi wa mabao 4-0.

Kocha Mkuu wa Serengeti Girls, Bakari Shime aliliambia gazeti hili kikosi chake kiko tayari kwa mchezo huo na wataingia uwanjani kwa ajili ya kupambana kusaka ushindi.

Shime alisema hawatabweteka na ushindi wa mechi iliyopita kwa sababu wapinzani wao wana kikosi imara na wanaweza kuingia tofauti kwenye mechi hiyo ya marudiano.

"Tumekamilisha maandalizi yetu, tumejipanga imara kuendelea kusaka ushindi, lengu letu ni kusonga mbele katika mashindano haya," alisema Shime.

Naye nahodha wa Yanga Princess, Amina Bilali alisema kwa sasa akili na nguvu zao wanazielekeza katika kuhakikisha wanamaliza msimu katika nafasi ya pili ya vita ya ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania wameiacha kwa Simba Queens na Fountain Gate Princess.

Amina alisema hawajakata tamaa katika ubingwa ila wanajiondoa kwa sababu ya tofauti kubwa ya pointi iliyopo dhidi ya timu hizo mbili zinazoongoza kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Msimu huu hatuna uhakika wa ubingwa kwa sababu ukiangalia aliyekuwa juu yetu (Fountain Gate) ametuzidi pointi sita na Simba Queens wametuzidi pointi saba, katika hali hiyo hatuwezi kujihakikishia ubingwa zaidi ya kupambana kumaliza nafasi ya pili," alisema Amina.

Yanga Princess juzi iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Tigers Queens na kuifanya ifikishe pointi 38 wakati Fountain Gate Princess wana pointi 44 na vinara Simba Queens wamejikusainyia alama 45.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Mercy Tagoe (kushoto), akijaribu kumtoka mlinzi wa Alliance Girls katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mo Arena, Bunju jijini Dar es Salaam. Simba Queens ilishinda mabao 3-0. **PICHA: SIMBA SC**

# *Azam FC yalalamikia uwanja mbovu*

Na Shufaa Lyimo

BAADA ya kupata sare ya mabao 2-2 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold FC iliyochezwa juzi, benchi la ufundi la Azam limesema ubovu wa Uwanja wa Sekondari Nyankumbu ulioko mkoani Geita umechangia matokeo hayo.

Msemaji wa Azam FC, Thabit Zakaria alisema mchezo huo ulikuwa mgumu na wenye ushindani, lakini wanashukuru kugawana pointi na wenyeji.

"Mchezo wetu umeharibiwa kutokana na hali ya uwanja ilivyokuwa, tulitarajia kupata matokeo zaidi ya haya," alisema Zakaria.

Hata hivyo alisema washambuliaji wake walishindwa kutumia vyema nafasi walizozitengeneza katika kipindi cha pili na kuruhusu wapinzani kufunga bao la kusawazisha.

Kikosi cha Azam tayari kimeanza safari ya kuelekea Bukoba kwa ajili ya mchezo mwingine wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar utakaochezwa Mei 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kaitaba.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 01/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 4904 | Juventus vs Venezia | 1.23 | 5.69 | 10.66 |
| 14:00 | 2117 | Spartak Moscow vs Kryliya Sovetov | 2.02 | 3.27 | 3.57 |
| 14:00 | 4933 | Celtic vs Rangers | 1.87 | 3.49 | 3.93 |
| 14:00 | 5879 | Troyes vs Lille | 3.44 | 3.24 | 2.10 |
| 14:30 | 5692 | Royal Antwerp vs Union Saint Gilloise | 3.18 | 3.43 | 2.13 |
| 15:00 | 5512 | Elche vs Osasuna | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 15:15 | 2520 | FC Sion vs BSC Young Boys | 4.08 | 4.08 | 1.71 |
| 15:30 | 4882 | GO Ahead Eagles vs Vitesse Arnhem | 2.82 | 3.32 | 2.36 |
| 15:30 | 5347 | PSV Eindhoven vs Willem II Tilburg | 1.12 | 7.69 | 16.75 |
| 16:00 | 2493 | Mjallby vs Helsingborg | 1.82 | 3.26 | 4.09 |
| 16:00 | 2736 | Empoli vs Torino | 2.67 | 3.32 | 2.47 |
| 16:00 | 3113 | AC Milan vs Fiorentina | 1.61 | 3.90 | 4.94 |
| 16:00 | 3642 | Lorient vs Reims | 2.24 | 3.13 | 3.23 |
| 16:00 | 3889 | Montpellier vs Metz | 1.73 | 3.74 | 4.39 |
| 16:00 | 4246 | Degerfors vs Elfsborg | 4.10 | 3.90 | 1.67 |
| 16:00 | 4693 | Everton vs Chelsea | 4.48 | 3.58 | 1.73 |
| 16:00 | 4983 | Monaco vs Angers | 1.36 | 4.87 | 7.36 |
| 16:00 | 5125 | Kayserispor vs Besiktas | 3.53 | 3.58 | 1.95 |
| 16:00 | 5246 | Tottenham vs Leicester | 1.44 | 4.57 | 5.97 |
| 16:00 | 5275 | Alanyaspor vs Yeni Malatyaspor | 1.26 | 5.57 | 9.56 |
| 16:00 | 5859 | Brest vs Clermont Foot | 2.22 | 3.33 | 3.08 |
| 16:30 | 5966 | FK Khimki vs Ufa | 2.36 | 3.12 | 2.98 |
| 17:00 | 5165 | Randers vs Brondby | 2.04 | 3.33 | 3.53 |
| 17:00 | 5738 | Bohemians vs Pardubice | 1.92 | 3.53 | 3.93 |
| 17:00 | 5805 | Olympiakos vs PAS Giannina | 1.31 | 4.79 | 9.79 |
| 17:15 | 5005 | Granada vs Celta Vigo | 2.76 | 3.16 | 2.56 |
| 17:30 | 2415 | FC Basel vs FC Zurich | 2.37 | 3.54 | 2.69 |
| 17:30 | 3677 | Vitoria Guimaraes vs Santa Clara | 1.97 | 3.34 | 3.73 |
| 17:30 | 4670 | FC Luzern vs Lausanne-Sport | 1.81 | 3.74 | 3.94 |
| 17:45 | 1900 | Fortuna Sittard vs Feyenoord | 6.54 | 4.85 | 1.39 |
| 18:00 | 1996 | RB Salzburg vs Josko Ried | 1.14 | 6.79 | 12.61 |
| 18:05 | 4348 | Bordeaux vs Nice | 3.43 | 3.58 | 1.98 |
| 18:30 | 1884 | West Ham vs Arsenal | 4.08 | 3.51 | 1.82 |
| 18:30 | 3880 | GIF Sundsvall vs AIK Football | 5.23 | 3.73 | 1.56 |
| 18:30 | 5617 | BK Hacken vs Varbergs Bois | 1.63 | 3.63 | 4.75 |
| 19:00 | 5061 | Udinese vs Inter | 5.36 | 4.17 | 1.53 |
| 19:00 | 5390 | Akhmat Grozny vs CSKA Moscow | 3.02 | 3.22 | 2.29 |
| 19:30 | 1690 | Rayo Vallecano vs Real Sociedad | 3.11 | 3.06 | 2.37 |
| 19:30 | 5143 | Anderlecht vs Brugge | 2.37 | 3.48 | 2.73 |
| 20:00 | 3163 | Moreirense vs Boavista | 2.19 | 3.23 | 3.23 |
| 20:00 | 4204 | New York City vs San Jose Earthquake | 1.40 | 5.08 | 6.70 |
| 20:00 | 5509 | Slavia Prague vs Viktoria Plzen | 1.64 | 3.73 | 5.45 |
| 20:30 | 3806 | Galatasaray vs Sivasspor | 1.91 | 3.44 | 3.83 |
| 20:30 | 5541 | Goeztepe vs Caykur Rizespor | 2.04 | 3.44 | 3.39 |
| 21:00 | 4844 | Waalwick vs Groningen | 2.75 | 3.15 | 2.51 |
| 21:45 | 2801 | Marseille vs Lyon | 2.24 | 3.48 | 2.93 |
| 21:45 | 4683 | Roma vs Bologna | 1.44 | 4.47 | 6.16 |
| 22:00 | 2913 | Barcelona vs Mallorca | 1.36 | 4.98 | 7.57 |
| 22:30 | 2425 | Sporting Lisbon vs Gil Vicente | 1.32 | 4.98 | 8.37 |
| 23:00 | 1664 | Nashville SC vs Philadelphia Union | 2.33 | 3.07 | 3.27 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Mei 1, 2022

Nipashe



Klopp: Liver timu sahihi kwangu UKURASA 21

# Simba, Yanga hakuna mbabe

## Ni sare ya pili kwa vigogo hao msimu huu huku...

**Adam Fungamwangowa na Saada Akida**

KWA mara nyingine tena, mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya watani wa jadi Yanga na Simba iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam ilimalizika kwa suluhu.

**Mechi ya mzunguko wa kwanza kwenye uwanja huo huo iliyochezwa Desemba 11, mwaka jana pia timu hizo zilitoka sare ya bila kufungana.**

Kwa matokeo hayo, Yanga inaendelea kukaa kileleni ikiwa na pointi 55 huku Simba nayo ikiendelea kung'ang'ania kwenye nafasi ya pili kwa pointi zake 42 kibindoni, lakini ikiwa na mechi moja mkononi.

Ilikuwa mechi ya wazi, kila timu ikijiachia kwa kucheza pasi na haukuwa mchezo wa kutumia nguvu sana kama ambavyo ilivyozoeleka huko nyuma.

Hata hivyo ni mechi itakayoingia kwenye rekodi ya kutokuwa na mashambulizi ya hatari kubwa kama zinavyokuwa mechi nyingine.

Kwa matokeo hayo, timu hizo zinamaliza msimu huu wa ligi bila kutambiana, huku Yanga ikiendeleza rekodi ya kutopoteza mechi yoyote msimu huu mpaka sasa.



Winga wa Simba, Bernard Morrison (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: MTANDAO**

Simba ndiyo iliyoanza mechi hiyo kwa kasi, na sekunde ya 17 walikuwa tayari wameshabisha hodi golini mwa Yanga lakini golikipa, Djigui Diarra alilazimika kufanya kazi ya ziada kuruka juu na kuudaka mpira uliokuwa unakwenda kwenye kichwa cha straika wa mabingwa watetezi, Chris Mugalu.

Dakika ya pili Yanga ilijibu shambulio, beki wake wa kushoto, Kibwana Shomari alipoambaa na mpira kwenye wingi ya kushoto, kabla ya kumimina majaro ambayo, Joash Onyango alitaka kupiga kichwa, lakini aliteleza na kuufanya mpira huo kupita.

Wakati mashabiki wa Yanga wakitarajia wachezaji wao watautapata mpira huo na kuukwamisha wavuni nao waliukosa na kutoka nje ikawa kona.

Hatari nyingine kipindi cha kwanza ilikuwa ni dakika ya 15 pale Feisal Salum alipomegewa pande na Khalid Aucho, akaachia shuti kali kama kawaida yake, lakini ukatoka nje kidogo ya lango la Simba.

Kwa kipindi chote cha kwanza hakukuwa na timu iliyopelela msukosuko wa maana langoni kwa mwenzake, huku mpira ukichezwa kati zaidi. Viungo wa Simba na Yanga walionekana kuonyeshana ufundi.

Simba ilikuwa ikijenga mashambulizi yake taratibu kwa pasi fupi fupi na kulazimisha kupita kati wakati Yanga ilikuwa ikijenga mashambulizi yake kwa kasi, ikimtumia winga wa upande wa kulia, Jesus Moloko na beki, Kibwana kwa upande wa kushoto.

Mabeki, Dickson Job na Bakari Mwamnyeto wa Yanga walifanya kazi kubwa kuwadhibiti Clatous Chama, Mugalu na Pape Sakho, huku Henock Inonga 'akikichafua' na Fiston Mayele. Mwamuzi Ramadhani Kayoko alilazimika kuwazawadia kadi za njano, Diarra na Bernard Morrison kwa kutunishiana misuli, lakini pia Inonga na Moloko kwa kusukumana.

Angalau kipindi cha pili kulionekana hatari kubwa chache, hasa ya dakika ya 71, ambapo baada ya kumdhibiti sana, Inonga alimsahau Mayele, ambaye alipenyezewa pande safi na Saido Ntibazonkiza, akaachia shuti kali ambalo mashabiki wengi wa Yanga waliamini mpira ulikuwa umekwama wavuni, lakini uliparaza nyavu za pembeni ukiwa nje.

Jaribio hilo lilijibiwa dakika mbili baadaye kupitia kwa Mugalu aliyeruka juu na kupiga kichwa faulo ya Kapombe, lakini mpira ukadakwa na Diarra.

Mkude nusura asababishe timu yake ifungwe, aliporudisha mpira wa kichwa kwa, Aishi Manula dakika ya 75, lakini haukufika na kuwahiwa na mabeki wa timu yake pamoja na wachezaji wa Yanga, ikawa kizazaa ambacho hakikufanikiwa kuzaa bao.

Simba ingeweza kuandika bao dakika ya 10 baadaye, ilipotokea patashika kwenye lango la Yanga, lakini Mugalu na Denis Kibu aliyeingia badala ya Morrison mashuti yao yaliwababatiza mabeki na kuokolewa.

Kwenye mechi hiyo Simba iliwatoa Pape Sakho, Chama, Morrison na Saido Kanoute aliyeumia na kuwaingiza Rally Bwallya, Kibu Denis, John Bocco na Mzamiru Yassin, huku Yanga ikiwatoa Moloko, Fei Toto na Ntibazonkiza, nafasi zao kuchukuliwa na Salum Aboubakar, Farid Mussa na Denis Nkane ambao pamoja na kuonekana kuongeza nguvu kwenye timu zao, lakini hawakubadilisha ubao wa magoli.

Mashabiki wa vigogo hao wa soka nchini wamejitokeza kwa wingi uwanjani kushuhudia mtanange huo hakuna upande ambao unaweza kusema umeuzidi mwingine.

Ulinzi waimarishwa nje na ndani kutokana na polisi kuonekana wakiwa makini na kazi ya kukagua tiketi na kuangalia usalama wa mashabiki waliofika uwanjani .

Timu zote ziliwasili uwanjani saa 9:37 mchana kwa kuingia kwa wakati mmoja lakini Yanga wao walitangulia kukanyaga nyasi ambapo walifika uwanjani saa 10:12 jioni.

Kwa upande wa Simba wameingia ndani ya uwanja saa 4:20 jioni kwa ajili ya kuanza kufanya mazoezi mepesi kujiandaa na pambano hilo.

Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco alikabidhiwa tuzo yake ya kocha bora wa Machi sambamba na kiungo wa Wekundu wa Msimbazi , Clatous Chama alitangazwa kuwa bora wa mwezi huo.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally aliamsha shangwe kwa mashabiki wa timu hiyo kwa kitendo cha kuwamwangia maji ikiwa ishara ya furaha kwa mashabiki wao.

Hata hivyo, mashabiki wa Simba walimzomea Mayele baada ya kuiga kitendo cha beki wa Wekundu wa Msimbazi, Henock Inonga kuwataka mashabiki washangilie wakati vikosi vya timu hizo vikijiandaa kupiga picha.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >